# Bartimayo Kipofu

Amina. Hebu tuseme "Bwana asifiwe," kwa njia hii kwa ajili ya wimbo huo mzuri. [Kusanyiko linashangilia—Mh.] Je, hiyo si ni kweli? "Yesu ajapo, mambo yote yanabadilika basi," sivyo? Utusitusi wote unaondoka, giza.

2 Na tuna furaha sana kwamba Yesu ameahidi, kwamba popote wawili watatu walikusanyika kwa Jina Lake, kwamba Yeye angekuja. Kwa hiyo tunajua ya kwamba atakuwa hapa usiku wa leo, tayari yuko hapa, kwa sababu tumekusanyika katika Jina Lake.

3 Kila usiku, baada ya kama saa sita, ninapojirudia mwenyewe vizuri, mtu fulani huniambia, mvulana wangu au mke wangu, mmojawapo, "Ulichukua muda mrefu sana usiku wa leo, Billy. Hao ni watu wanaofanya kazi. Unaona ni wangapi wanaokuja. Ni baridi sana katika hema hiyo." Kwa hiyo nitajaribu kutoka mapema kidogo, nikiweza, basi. Kwa hiyo ombeni pamoja nami, na mniombee, nami nitafanya vizuri niwezavyo kuharakisha usiku wa leo.

4 Vema, ninashukuru sana. Tunakosa kitanda kimoja, kiti kimoja cha magurudumu usiku wa leo (Mungu asifiwe; hilo ni jema.) tangu jana usiku. Natumaini utakuwa ni usiku wako, usiku wa leo, dada, na usiku wako pia, dada, usiku wa leo, kwamba hutalazimika kuwa kwenye kiti cha magurudumu au kitanda kidogo kesho usiku. Nami natumaini kwamba wao, si hata mmoja wenu wala. . .mtakuwa mmeketi huko nyuma kwenye kusanyiko kesho usiku, au katika kanisa lenu wenyewe, au popote mwendapo.

5 Sasa, kwa hawa waongofu wapya ambao ndio kwanza waongoke mkutanoni, msikae tu bwete. Tafuteni kanisa zuri la kuendea. Angalieni huku karibu. Ikiwa unatoka katika bonde hili na maeneo ya karibu hapa mahali fulani, waangalie wachungaji hawa wanaokuja hapa jukwaani, na wanatusaidia katika mkutano. Wanaamini katika aina hii ya huduma. Kwa hiyo nenda kwenye kanisa lao na kuwaambia kwamba unataka kuwa mshiriki huko.

6 Na kama ningekuwa katika ujirani huu mahali fulani, au karibu nao, ningekuwa mshiriki wa kanisa lao, maana ninawathamini. Nao wenyewe wameketi papa hapa jukwaani, usiku, kumwacha kila mtu ajue yale wanayoamini. Na ikiwa uko nje ya mji, kutoka mahali pengine, jitafutie kanisa zuri mahali fulani, kanisa zuri linalohubiri Injili na kuamini katika uponyaji wa Kiungu. Sasa, kama wewe. . .

7 Sijui makanisa mengi sana huku juu. Najua mengine huko chini njia ile nyingine. Ninajua kuhusu Angelus Temple,

kanisa zuri sana. Hilo ni moja kwa moja huko Los Angeles. Na ninamjua Dk. Teeford na—na—na Rolf McPherson, na—na Daktari Cummings, na ndugu hao wo—wote wazuri sana; kanisa zuri sana. Watu wa Foursquare ni wazuri sana. Kama unaishi karibu na hilo hekalu, mbona, kumbuka hilo tu.

8 Ninawafanyia mikutano kote nchini; Ndugu Beard kutoka magharibi ni rafiki yangu msiri. Nami nina mikutano yao mikubwa na kadhalika, watu wazuri sana. Na Rolf McPherson, nafikiri, ni mmoja tu wa watu wazuri sana ambao nimewahi kukutana nao; mtu mzuri sana.

9 Kisha kuna Ndugu O. L. Jaggers kutoka Kanisa la Ulimwengu kule chini, mtu mwingine mzuri. Nimekuwa na mikutano kwa ajili yake, nasi tumekuwa na ushirika mzuri pamoja.

10 Sasa, kuna ugomvi kidogo kati ya hayo makanisa, lakini hilo lisiwasumbue. Wote wako sawa. Wao ni . . . Hiyo ni—hiyo ni sawa; hao ni ndugu. Wako sawa, wote ni watu wazuri, kila mmoja wao. Hiyo ni kweli. Hamna budi kuwa na ugomvi kidogo wakati mmoja kuninii . . . Vema, kwa namna fulani wanafikiri wao ni washindani, kidogo kuwadumisha wa kiroho. Wasipoliacha liende mbali zaidi ya hapo, itakuwa sawa.

11 Lakini ninampenda sana Ndugu Jaggers, na ninampenda Ndugu Teeford, na Ndugu McPherson, na hao wote. Wote wamekuwa ndugu wapendwa sana kwangu. Nami ninawapenda wote. Kwa hiyo mabishano yao madogo, mbona, hayo—hayo ni sawa; hayo hutokea tu hata katika familia, mnajua. Na kwa hivyo, familia ya Mungu haiendi kwa urahisi zaidi, inavyoonekana, kuliko sisi wengine twendavyo. Kwa hiyo wote wako sawa, wote wawili. Wako sawa, au, wote. Ni jamaa wazuri.

12 Nami ninaamini kuna Ndu—Ndugu A. A. Allen akiendeleza uamsho huko mbali mahali fulani Los Angeles kule chini. Simjui sana mtu huyo. Nimesikia habari zake, lakini simjui. Lakini yeye ni ndugu ambaye anafanya ibada za uponyaji. Na—na kama kuna yeyote huko chini katika sehemu hiyo, mbona . . . Bila shaka, Ndugu Allen ni mwinjilisti kama nilivyo mimi. Yeye hana kanisa lolote maalum.

13 Halafu kuna Ndugu Leroy Kopp kule chini ambaye ana kanisa. Na—nami ninamjua vizuri sana, ndugu Mkristo mzuri sana. Na, loo, kuna makanisa mengi mazuri tu kote hapa unayoweza kuhudhuria.

14 Kwa hiyo uwe na hakika, kati ya hayo makanisa yote mazuri, unapaswa kupata moja mahali fulani. Basi ujitafutie kanisa la nyumbani, na uingie ndani na kuwaambia ya kwamba unataka kuwa mshiriki wa kundi lao la waaminio.

15 Halafu basi kumbuka, kisha nenda kwa makanisa mengine na—na kufanya ushirika nao, pia. Usimkatae kamwe mtu yeyote kama Mkristo, haijalishi kama yeye si Mpe—Mpentekoste, ama

kama yeye ni Mbaptisti, ama Mmethodisti. Kumbuka, yeye ni ndugu yako hata hivyo. Unaona? Hiyo ni kweli. Dumu moja kwa moja nalo.

16 Ikiwa hujisikii hivyo, basi unapaswa kurudi. Unaona? Hiyo ni kweli. Unapaswa kurudi kwa sababu hukuenda mbali vya kutosha, unajua. Ikiwa wewe tu. . .

17 Nilikuwa nikisimulia hivi majuzi kuhusu ndugu Mmethodisti, rafiki yangu. Naye. . .tulikuwa na ushirika mwingi pamoja. Naye alikuwa akichunga kanisa la Methodisti huko New Albany. Na sisi sote tulizaliwa huko Kentucky. Nilizaliwa katika bonde moja naye alikuwa kwenye lingine. Hiyo ni karibu jinsi tulivyo na maelekezo yetu huko chini. Na hivyo. . .

18 Basi vema, nilimwita Ndugu Lum. Jina lake lilikuwa Edwards. Na kwa hivyo, kama ningepata mwongofu, aseme, "Sasa, Ndugu Billy," akasema, "Mimi. . .Baba na mama yangu walikuwa Wamethodisti nami. . .kwa hiyo mimi kamwe si—si—siwezi kuendea kuzamishwa. Na—na—nataka uninyunyizie."

19 Sasa, ha—ha—hangenifanya mwanachama mzuri huko juu. Kwa hivyo nasema, "Hebu nikwambie. Nina mmoja wa ndugu wazuri sana huko New Albany, jiji lililo tu chini yangu, maili tatu, naye ana. . .Yeye ni mchungaji wa kanisa la Kimethodisti la kiroho kweli." Ningesema, "Yeye ni mtu mzuri." Nilisema, "Kidogo ni kukavu, hakuna maji mengi karibu na hapo." Lakini nikasema, "Na—nakwambia, unapaswa kushuka umwendee. Sasa, nitakupeleka kwake."

20 Huyo alikuwa mwongofu wangu aliyetaka kuwa Mmethodisti. Kama yeye alikuwa na mmoja ambaye alitaka kuwa Mbaptisti na alitaka kuzamishwa kweli, angesema, "Vema sasa, kamwe hutanifanyia mfuasi mzuri, bali nina rafiki mzuri huko Jeffersonville, maskanini, jina lake Billy. Acha nikwambie, Billy atakuzamisha. Atakushikilia tu hadi kila kiputo kimeninii, kimeacha tu kutoka; bali ni mvulana mzuri."

21 Kwa hiyo hiyo ndiyo aina ya ushirika tuliokuwa nao. Ningemtania, niseme, "Ni kukavu sana huko kwake kwa sababu hana maji mengi kule New Albany, mwajua." Na kwa hivyo angesema kulikuwa chepechepe sana huko hata nikawazamisha. Lakini tulikuwa na ushirika, Methodisti na Baptisti. Nami ningeshuka, nimhubirie; angekuja, anihubirie.

22 Sasa, kama Wamethodisti na Wabaptisti watafanya hivyo, hakika hawa wengine wanaweza kufanya hivyo. Hiyo ni kweli. Kwa hiyo sisi sote ni ndugu katika Kristo Yesu, mnaamini hilo? Amina. Hilo ni zuri sana.

23 Sasa, tutalifungua Neno Lake. Basi nitaiweka hii saa yangu hapa ili nijue sitaenda sana. Mnaona? Sasa Mpenzi, usinikemee baada ya ibada hii. Unaona? Vema, nitajipimia wakati usiku wa leo, nikiweza.

24 Sasa, loo, yeye hanikemei, namtakia heri. Nilikuwa niende, kusema hivyo. Yeye huniambia tu, "Sasa, Billy, unajua hao ni watu wanaofanya kazi na hawana budi kuharakisha." Nami ninajua ni nini. Hiyo ni kweli.

25 Kwa hivyo tuwe katika maombi, kila mtu aombe sana. Pia kumbukeni, siku chache zaidi usiku sasa, itatubidi kuondoka California, jiji lenu la kupendeza hapa, au jimbo la kupendeza, na kurudi Louisiana. Ninatoka hapa kwenda kwenye mkutano huko Louisiana, na labda hivi karibuni sana nitarudi kwenye nchi za ng'ambo tena katika safari ndefu ya huko ng'ambo.' Kwa hiyo tuzungumze tu na Mwandishi sasa kabla hatujasoma Neno Lake?

26 Baba yetu wa Mbinguni, tunakuja Kwako kwa unyenyekevu katika Jina la Mtoto Wako mpendwa, Bwana Yesu, kukushukuru Wewe na kukusifu kwa yote uliyotufanyia.

27 Safari hii ndogo ya miaka michache ya ushirika pamoja na Wewe, jinsi mioyo yetu inavyofurahishwa kwa sababu tumekuona ukiokoa wenye dhambi na kuwajaza na Roho Wako Mtakatifu, kufanya wahudumu wa Injili kutoka kwao, kuwaondoa makahaba mitaani, kuwafanya wanawake halisi. Loo, jinsi tunavyokushukuru kwa ajili ya jambo hilo.

28 Kukuona ukichukua hao wagonjwa waliolazwa kitandani, wakati madaktari Wako wapendwa wamewakatia tamaa, na kusema, "Hakuna cha zaidi kinachoweza kufanywa; watakufa," na kukuona ukiwainua moja kwa moja wakawa watu wakamilifu, wenye afya njema, tunashukuru sana kwa ajili ya jambo hili, Baba, na ni vigumu kwetu kulielezea kwa maneno ya kibinadamu. Lakini pokea tu ibada yetu ya mioyo yetu tunapomimina nafsi zetu Kwako katika shukrani.

29 Na sasa, Baba, si utatufungulia Neno Lako usiku wa leo na uje ukae nasi kwa muda? Na uwaokoe wote ambao hawajaokolewa, na uwajaze Roho Mtakatifu wale ambao hawana Huyo usiku wa leo. Nasi pia tunaomba, Baba, ya kwamba utamponya kila mgonjwa aliye katikati yetu.

30 Tuna furaha sana kusikia shuhuda za jana usiku za yale uliyofanya. Nami naomba ya kwamba ikiwezekana, utupe sehemu maradufu usiku wa leo na umponye tu kila mtu aliye katika Uwepo wa Kiungu. Kwa kuwa tunaomba katika Jina la Yesu, Mwanao. Amina.

31 Sasa kumbukeni, msingi wa mkutano . . . Ni vigumu kufanya kazi. Na siku moja, kama ninyi nyote mnavyojua kutokana na ono, nanyi kutoka kule chini karibu na Los Angeles, kwamba siku moja huduma hii itaninii . . . Nitaisimamisha Marekani. Mnaona? Na—na halafu . . . Siwezi sasa kwa sababu watu wanapokuja, inaendelea tu kufanya kazi.

32 Lakini siku moja itakoma, wakati maskini mama mmoja atakapokuwa jukwaani amevaa nguo ya kahawia amemshika

mtoto mkononi mwake. Naye atakuwa na nywele nyeusi, naye mtoto amefunikwa blanketi nyeupe. Na huo utakuwa ndio mwisho wa huduma ya aina hii kwangu Marekani mpaka Bwana Yesu atakapoiitisha.

33 Lakini itakuwa kwenye nchi za ng'ambo. Mnaona? Humu ndani nitawaita tu watu na kuendeleza mistari ya maombi na kuwaombea. Wamarekani, ni vigumu sana kwao kuona. Wamekuwa na mengi sana katika jina la mambo ya kimbinguni, kwa namna fulani wanasita, wanayatilia shaka. Hawawezi kujiepusha.

Wamarekani wameshindiliwa mambo sana. Unaona, mmoja anasema, "Vema, Daktari Jones anasema hicho ni kiinimacho."

"Vema, mchungaji wangu alisema alikuwa mlokole."

"Vema, nawaambia. Nanii . . . mimi . . . Mchungaji wangu alisema ni ibilisi."

34 "Vema, mchungaji wangu hajui awazie nini kulihusu." Mnaona? Na wao ni wachunga kondoo. Na ni sawa. Wao ni . . . Mnaona? Lakini unachofanya, unategemeza hitimisho lako kwenye uamuzi wao. Una uamuzi wako mwenyewe wa kufanya. Unaona?

35 Kwa hivyo jambo ni kwamba: Jambo moja—jambo moja katika milki ya mambo ya kimbinguni kama hilo linaweza kutokea nchini India, na kila kilichopo kitainuka na kuponywa.

36 Nilimwona mtu mmoja akija jukwaani barani Afrika. Vema, walimwongoza kwa mnyororo shingoni mwake, wakamleta jukwaani namna hiyo. Naye mtu huyo akaambiwa alitoka kabila gani, na Roho Mtakatifu.

37 Naye Mwislamu alikuwa ndio kwanza apite, alikuwa amefanya jambo lile lile: kamwambia daktari aliyemwendea, na yote kuhusu hilo. Nao hao watu wakilia tu, karibu kila Mwislamu pale, akamjia Kristo wakati uo huo. Vema, mwenyeji huyu aliponywa na kupata afya na akaambiwa mambo hayo.

38 Waongofu elfu thelathini wakamjia Kristo na uponyaji wa uhakika elfu ishirini na tano ukafanyika kwa muda wa dakika moja. Hata walichukua malori na wakayajaza hayo magongo, na vitanda vikuukuu, na viti vya magurudumu, na fimbo, na marungu waliyotembea nayo, ili kuyaondoa uwanjani.

39 Na zaidi ya mwaka mmoja kutoka wakati huo, gazeti la Durban liliandika makala kuhusu mikutano hiyo, na kusema kwamba kabila moja, Waswazi kule juu, kwamba walichukua, nasahau ni malori mangapi ya bunduki, na saa, na vitu walivyokuwa wameiba. Walijitolea kabisa. Hawakutaka kujihusisha tena na dhambi.

40 Wala haikukubidi kuwaambia hao watu, waliokuwa wameketi pale uchi wa mnyama, wanaume, wanawake, na wote,

haikukubidi kuwaambia, "Vaeni nguo"; waache tu wampokee Kristo. Watavaa . . .

Inaonekana kana kwamba kwa namna fulani wanampoteza huku Marekani, sivyo? Hmm. Hiyo ni kweli.

41 Lakini ilikuwa ni ukafiri sana. Hili linasikika fidhuli kabisa. Da- . . . mama aliyeketi si mbali sana, angalau, kama mama huyu kwenye kiti cha magurudumu anavyoketi, alijifungua mtoto, huku ameketi pale pale, naye akamnyanyua tu. Na yalikuwa ni hayo tu. Mnaona? Nao hawaoni hilo. Na . . . huko juu katika makabila . . .

42 Lakini watu hao rahisi, hawahoji kamwe. Hawahoji. Wanaona jambo fulani likifanywa, hilo linawatosha, kila mmoja wao. Waambie tu, na kila mmoja wao atasimama na kuacha ninii zao . . . wengine wanaweza . . . labda hawezi kutembea, naye anajaribu kupiga hatua. Ndipo muda si muda mwajua, hapo anatimua mbio. Na huyu hapa mwingine anakuja hivi. Naye akimwona huyo akienda, huyo anaenda zake. Na kisha, muda si muda mwajua, ni—ni kusanyiko moja tu kuu. Hamna lingine. Hivyo ndivyo tu inavyokubidi kukaa. Yote yameisha basi.

43 Ndipo nikatoa wito wangu wa madhabahuni, nao makafiri watupu elfu thelathini, ambao walikuwa hawajajua lolote kuhusu Yesu Kristo, wakamkubali wakati mmoja na kuvunjia sanamu zao ardhini mpaka ilionekana kama dhoruba ya mavumbi karibu na mahali wangekuwa.

44 Lakini Wamarekani, sisi huku Marekani, loo, tunashangaa, "Sasa, si—sio hasa tu . . . yeye si wa kanisa langu." Na, "Si—sijui kuhusu hilo. Sasa, nawaambia. Mimi—mimi ni mtu mwenye akili sana. Nina elimu." Ungekuwa afadhali kama hukuwa nayo, iwapo hivyo ndivyo unavyofanya. Hiyo ni kweli.

Naam, inatubidi tu kuvumilia mambo hayo. Sisi ni ustaarabu mkubwa, lakini nahofu tuko mwisho. Um-hum.

45 Vema, katika Kitabu, katika mlango wa 18 wa Luka Mtakatifu, na kifungu cha 35, kwa ajili ya kusoma tu, na mazungumzo ya dakika chache tu. Basi nitaangalia saa yangu ya ukutani hapa, na mara inaposema saa tatu tutaacha tu na kuanza mstari wa maombi ili tuweze kuondoka ifikapo saa tatu na nusu, ikiwezekana: kifungu cha 35, sasa, cha mlango wa 18 wa Luka Mtakatifu:

> *Ikawa alipokaribia Yeriko, . . . mtu mmoja kipofu alikuwa ameketi kando ya njia akiomba sadaka:*

Bwana na aongeze baraka Zake kwenye Neno Lake.

46 Sote tunayafahamu Maandiko haya. Na wakati wa usiku kama huu, hujaribu kuhubiri, kwa sababu ni . . . ule upako . . . Nimekuwa alasiri yote nikiombea tu upako ili kuona maono yamekaribia. Na halafu basi—basi ninapoingia hapa na kuanza

kuhubiri kabisa, basi muda si muda mwajua, hayo yanatoweka. Ndipo basi ninaninii . . . una wakati mbaya sana.

47 Kwa hivyo inanibidi tu kuzungumza kidogo, kwa namna fulani kupata hisia za umati na kuwafanya wote watulie, na kila roho. Zaidi sana sio watu kadiri zilivyo roho, kuzituliza. Ndipo unaweza kuanzisha mstari wa maombi. Unaona?

48 Na sasa, hebu tuwe tukiyawazia mandhari haya usiku wa leo. Huko nyuma, hii ilikuwa tu mwishoni kabisa mwa huduma ya Yesu.

49 Jana usiku tulikuwa tunazungumza juu ya mwanzo, jinsi ambavyo Mungu alikuwa amempa maono ya kuondoka na kwenda zake, halafu . . . kwa sababu rafiki Yake alikuwa anaenda kufa, naye Mungu alikuwa akitaka kuonyesha nguvu Zake kupitia Mwanawe, Kristo, kumfufua mtu huyu.

50 Sasa, usiku wa leo tutakaribia kutoka kwenye mtazamo mwingine, mwishoni mwa huduma Yake. Naye alikuwa amefanya miujiza mingi kote nchini. Ingawaje, ilikuwa wakati huo, kama ilivyo siku hizi, haidhuru ni miujiza mingapi ingefanywa, bado kuna watu ambao hawangeamini.

51 Na kwa hivyo, onyesho letu linafunguka usiku wa leo kwenye jambo la kusikitisha sana. Ni kipofu naye ameketi, amejikunyata.

52 Hebu tuwazie wakati sisi . . . Hebu tulichukue katika mchezo wa kuigiza. Na hebu tuwazie kwamba jua linashuka. Ni baada ya saa tisa alasiri, labda.

53 Na zile kuta kuu ndefu za Yeriko, mbona, kipofu huyu amejikunyata kando ya kuta hizi. Na ninii yake . . . Alikuwa ombaomba, tunaambiwa. Na jina lake lilikuwa kipofu . . . jina lake aliitwa Bartimayo; wengi wenu hulitamka Bartimayo; njia yoyote itakuwa sawa. Naye alikuwa . . . Matumaini yake . . . Labda alikuwa na kazi ngumu sana ya kupata riziki. Nasi tunafundishwa na wanahistoria kwamba alikuwa ameoa, alikuwa na familia. Lakini alikuwa na wakati mgumu kupata riziki kwa sababu aliomba, na kulikuwa na ombaomba wengi siku hizo.

Kulikuwako . . . Wenye ukoma walikuwa ombaomba. Loo, hilo pigo la kutisha la ukoma, hakuna mtu anayeweza kupita karibu nalo pasipo angalau kuwa na hisia za ajabuajabu.

54 Nimewaona. Nilikuwa nikifikiri kwamba ukoma huambukiza, kwamba unaweza kuambukizwa. Lakini huwezi kuambukizwa ukoma, mmoja kutoka kwa mwingine. Nimewakumbatia na kuwabusu, na chochote kile. Kwa hivyo hamwezi kuambukizana ukoma. Hu—husababishwa na lishe.

55 Na nimekuwa na wenye ukoma wasio na chochote ila vigutu tu vya mikono namna *hiyo*, wakivizungusha vigutu vidogo, wakijaribu kunikumbatia katika mstari wa maombi na

kadhalika; maskini wanawake wakongwe mitaani. Na wakati mwingine ukoma hula vidole vya miguu mpaka vinasimama tu kama dutu mkubwa, mkubwa *hivyo*, mweupe kabisa. Lakini tu, loo, mionekano ya kutisha ya ukoma. Ni kitu cha kuchukiza jinsi gani kuwa nao. Sayansi ya tiba bado haina dawa yake. Na ni kitu cha kuchukiza sana. Sio kitu kichungu, lakini ni . . . Inasikitisha sana kuona mtu ambaye amekatwa mikono, na kadhalika, na labda sehemu ya uso wao na masikio yao yameliwa na ukoma. Na inaonekana nyeupe, ni ya kutisha sana.

56 Basi kulikuwa na wenye ukoma wengi siku hizo, nao . . . hao watu wangelazimika kujitokeza asubuhi. Labda mtu ambaye angeweza kumudu kumpa mtu sarafu, labda yeye . . . mtu wa kwanza aliyekutana naye, alimpa sarafu. Hiyo ilitosha kwa siku hiyo. Asingeweza kumpa kila mmoja, kwa sababu ombaomba walikuwa kila mahali: ombaomba vipofu, na ombaomba viwete, na kulikuwa na wenye ukoma, na kila aina ya mateso ambao waliketi kote tu wakiomba. Hayo ndiyo mandhari ambayo Bwana wetu aliona alipokuwa hapa duniani.

57 Katika namna ya kimashariki, huko mashariki, hasa, haijabadilika sana. Mimi n- . . . nimekuwa huko mashariki, na kuwaona wanajimu, mamajusi, wameketi mtaani, wakikaza macho juu. Basi ni kama tu ilivyokuwa wakati Yesu alipokuja: wangali wamejifunga vitambaa vyao viunoni na vilemba vichwani mwao na kadhalika; daima ni wadadisi, na kutaka kuuliza maswali; na kuzungumza juu ya mambo ya kimbinguni; na kadhalika.

58 Na kwa hiyo, maskini mzee huyu kipofu, aliyeketi hapo, labda katika majira ya kupukutika mwakani na labda alikuwa anashangaa jinsi atakavyojipatia pesa zake za kipupwe. Nako huwa baridi sana huko chini.

59 Na—naye alikuwa ameketi kando ya barabara akiombaomba. Labda angekula leo, na kesho yake asiweze kula. Labda kesho yake asingeweza kula, na kisha anapata za kutosha kukipata tena.

60 Nakumbuka kule Bombay, kamwe sitasahau wakati tulipoingia kule, kulikuwa . . . Bombay, India, mahali fukara sana. Mnajua kwamba walipata uhuru wao wakiwa wamefilisika, ninii chache . . . karibu miaka mitano au sita iliyopita.

61 Na kuna watu milioni mia nne na sabini nchini India, lakini kuna mamilioni mengi, mengi sana yao ambao ni ombaomba. Walilala mitaani kama kuni, huko Bombay.

Nami ninakumbuka baada ya usiku wa kwanza, nao watu walijua mahali tulipokuwa tukikaa pale kwenye ile Hoteli ya Taj Mahal. Kesho yake asubuhi . . .

62 Nilikuwa na pesa ambazo zilikuwa pesa za Marekani. Nami ningechukua matoleo kwa ajili ya nchi za ng'ambo, na

kuyaweka akiba mpaka tulipopata za kutosha kwenda kule, kisha tunaenda kuhubiri Injili, kisha tunarudi na kufanya mikutano zaidi ya Marekani, ndipo nipate pesa za kutosha, niende na kuhubiri, kisha ningerudi.

63 Na kwa hiyo nilikuwa na pesa ambazo watu walikuwa wamenipa ili niwape watu. Na kwa hivyo nikashuka, nikawazia, "Vema, nitazibadilisha tu ziwe—ziwe Rupia za India." Na kwa hivyo nikaingia mtaani. Nami ninawaambia, karibu iwalazimu kuwa na kila . . . jeshi la kunitoa mtaani. Wangekukanyaga na kadhalika, wakikimbia juu yako, ombaomba, walipojua nilikuwa kule juu. Lilikuwa ni jambo la kusikitisha sana.

64 Kesho yake asubuhi wakati Bw. Baxter na wengineo walipokuja kunichukua niende kula kifungua kinywa, nami nikashuka kule, kisha mimi . . . Nikiisha kuwa huko, nilitazama nje, na kote kumejaa tu ombaomba.

65 Basi nikaenda huko nikiwa na lundo la hizi, rupia hizi. Hizo ni kama senti ishirini na nne kila moja; ambazo mtu ambaye ataenda kazini, mwanamke au mwanamume, mmojawapo, ataenda kazini karibu saa kumi alfajiri na kufanya kazi hadi saa nne usiku akiwa na kikapu kichwani mwake, amebeba zege akipanda vipandio vikubwa na kuimwaga ndani, zege mwilini mwao mwote na kila kitu, apate rupia kwa siku, naye anafurahia kuipata.

66 Na wanaweza kununua bizari, na hiyo karibu imetosha. Watu wakitembea mtaani, maskini tumbili wadogo wanaokufa kwa njaa wakiwafuata, wanatafuta-tafuta, waokote chochote wanachoweza kula. Ni wahitaji kweli.

67 Na kwa hiyo nikanyakua lundo la rupia hizi, nami nikasimama pale dirishani, nikizitupa nje namna *hiyo*. Nami nawaambia, ni ajabu hawakuuawa, rupia hizo tu. Huku watu wakipiga kelele na kuangukiana.

68 Vema, Wamarekani walikuwa wamenipa ili niwape, nihakikishe hazikuingia katika shirika fulani na mtu fulani azitumie na kadhalika, lakini moja kwa moja zilimfikia mtu binafsi. Hivyo ndivyo ninavyopenda kuzitoa, moja kwa moja kwa mtu ninayejua zinamfikia.

69 Vema, basi nilipoenda kula kifungua kinywa, ninawaambia kilikuwa kilio kimoja tu saa zote za usiku. Ingevunja tu moyo. Ningeenda dirishani, na hapo, akina mama wakiwa na watoto wao wachanga, mikono yao midogo, midogo, midogo sana, na mashavu yao yote yamebonyeka, matumbo yao madogo yamevimba kwa njaa, maskini mama angeweza kusimama kwa shida tu. Alikuwa akiombaomba kwa ajili ya mtoto wake. Haikuleta tofauti yoyote kama alikufa, maadamu asimwache mtoto afe kwa njaa.

70 Vema, utawapaje hao akina mama? Halafu kila mtu amesimama pande zote, na—na wenye ukoma na kila kitu,

kwa hiyo nilipoingia mle na kujaribu kula kifungua kinywa, ningeweza kuwasikia mchana kutwa na usiku kucha, huko nje wakipiga kelele "Padre."

71 Pa-. . .Vema, *padre* ni. . .Ni. . .Nafikiri ni neno la Kihispaniola ambalo linamaanisha "baba," au "wahudumu." Na kwamba, wao, wanalia tu hilo mchana na usiku. Nikawapa pesa zote nilizokuwa nazo, naitakia heri maskini mioyo yao. Ni—niliwahurumia.

72 Na kuwaona ombaomba wote. Ningesimama pale dirishani na kurudi nyuma. Wangeniletea kifungua kinywa changu: chungwa na biskuti kadhaa. Mara tu chai. . .na maskini ile chai chungu, nilikunywa chai nyingi sana mpaka ikawa ni "chai, chai." Naamini ungenidunga kwa kijiti, ningelitokwa na chai. Ni wakati wote tu, chai, chai, chai tu, kila saa chache. Nao wangeileta mle; nisingesema lolote kwa sababu ilikuwa kwenye bili ya hoteli. Mnaona? Ndipo basi ningechukua machungwa haya na biskuti na kwenda kule na kuwatupia hao akina mama na watoto wachanga. Loo, jamani. Ndipo nikaona. . .

73 Nikamwambia Billy Paul, kijana wangu, nikasema, "Sijui kama huyo jamaa asiye na mikono, ataziokotaje kamwe?" Hata, alikuwa akisukuma vidole vyake vya miguu, namna *hiyo*, kwenye vigutu vyake vya miguu yake. Ukoma ulikula miguu yake. Basi hatimaye tukamweka upande mmoja ambapo tungeweza kumwangushia rupia.

74 Unajua jinsi alivyoipata? Na hiyo mitaa ambapo ng'ombe wote wanapitia, na loo, jamani, ni vigumu sana kushikilia pua yako ili upite, akailamba kwa ulimi wake, naye huyo akateremka mtaani kwa hivyo vigutu, upesi tu alivyoweza, kuzisalimisha ili anunue bizari iliyotengenezwa kwa miguu ya kondoo, na kadhalika, akale.

75 Ndugu, nakwambia, mimi ni mwanadamu. Hilo—hilo nusura tu liniue, kuwaona hao watoto wachanga, ndipo nikawazia, "Rehema! Ee, Mungu, itaendelea muda gani zaidi?"

Na sisi hapa—sisi hapa, tutoke nje vya kutosha hapa kwenye uchochoro, kuwalisha watu, karibu.

76 Lakini angalieni hapa, najua hili liko nje ya njia iliyoandaliwa, somo langu. Ninataka kuwaambieni jambo fulani, niwaangushie tu hili. Juma lililopita nilipaswa kuhubiri lakini nataka tu kusema neno hili.

77 Angalieni, tunaenda kule na kumwambia mtu huyo kwamba yeye ni ndugu yetu. Vema, tunafanya nini? Tunatuma mtu huko, naye anamwona Mmarekani akishuka kwenye gari, kutoka kwenye mashua; anapitia hapo na gari zuri kubwa mno.

78 Yeye anakaa kwenye kibanda kidogo kikuukuu cha matope, mabua machache ya kitu fulani anacholima pale. Wajukuu wa—wake. . .Babu wa baba yake alilelewa katika ujinga. Baba yake,

yeye huyo hapo, watoto wake wanakuja vivyo hivyo. Mkewe atafulia kwenye kidimbwi hicho na yeye atabeba kidogo ili anywe kutoka kwenye kidimbwi hicho hicho.

79 Na ikiwa sisi ni ndugu, kwa usawa, kwa nini huyo huja amevalia vizuri? Na kama. . .Ninaona aibu kulisema, lakini mara nyingi unadadisi, na kumnyanyasa. Halafu ati unajaribu kumzungumzia Ukristo? Anashangaa.

80 Sasa, yaliyotukia, ukomunisti umeshuka na kumwambia yote ni ya uongo, kisha ukamletea uchumi wa uongo huko. Lakini ukimpa tumaini ulisema, "Naam, hivyo ndivyo wafanyavyo, hao ni ma—mabepari," na kadhalika. Na muda si muda mwajua. . .

81 Sababu ya kufanya hivyo ni kwa sababu tunaweka pesa zetu kwenye makopo ya bia na kofia na vitu kama hivyo, ndipo ikamlazimu mmishenari kuishi kwa senti moja inayokuja madhabahuni karibu mara moja kwa mwezi. Basi ndugu, tumepanda, nasi tutavuna tulichopanda. Kumbukeni tu hilo. Hakika.

82 Loo, jamani, ombaomba. Ninaweza kumwona mzee kipofu Bartimayo ameketi pale kando ya lango. Hebu tumchukue kwa dakika chache tu. . .kama hivyo, kama mtu binafsi. Hebu tuwazie tu tunamwona ameketi pale na tungeweza kupata kile alichokuwa akifikiria.

83 Nawazia alikuwa ameketi pale, akitetemeka, zile pepo, mikono yake michakavu ikining'inia chini. Hawezi kuona. Kama angeweza kufanyiwa upasuaji kwa ajili ya upofu wake, mbona, hakuwa na pesa za kufanya hivyo. Labda hawangeweza kumfanyia chochote, hao madaktari, kwa sababu nadhani ilikuwa mbali mno kwao, na hasa katika siku hizo. Kwa hiyo alikuwa akitetemeka.

Na ningemwazia akiwa mwaminio, angeweza kukumbuka yaliyopita, "Unajua nini? Nimeketi papa hapa karibu na ukuta huu."

84 Na moja kwa moja nje, kama yadi mia moja kutoka kwake, pale, ilikuwa ni barabara ile ile miaka mingi iliyopita, kule, shujaa mkuu Yoshua alizunguka kuta wakati hizo kuta zilipoanguka. Sio ila tu yadi mia chache kutoka pale hadi pale ambapo Yoshua, akipanda kuelekea langoni siku moja, Jemadari wa jeshi la Bwana aliposimama ameuinua upanga wake juu. Lakini masalale, hizo siku zimepita.

85 Yeriko ule ule ambapo huyu kipofu aliketi; ninaweza kumwazia Bartimayo akisema, "Loo, laiti ningalikuwa nikiishi wakati huo, wakati Yehova alikuwa halisi kwa watu, wakati Yehova kweli alitufanyia miujiza. 'Lakini hizo siku zimepita,' kuhani asema. 'Hiyo ilikuwa mamia ya miaka iliyopita. Yehova hafanyi mambo haya siku hizi.'"

86 Na halafu, pia, moja kwa moja kwenye barabara iyo hiyo, Eliya na Elisha walishuka wamekumbatiana, wakienda zao Yordani, ambapo waliyapiga maji, ndipo hayo maji yakagawanyika huku na huko, wakavuka penye nchi kavu.

87 Ninaweza kuwazia kipofu Bartimayo akisema, "Loo, laiti ningaliishi tu katika siku hizo, wakati wale manabii wakuu, wenye nguvu waliposhuka kwenye barabara hiyo kuu, pale. Ningaliwakimbilia, na kusema, 'Nabii wa Mungu, unirehemu, na nipate kuona.' Lakini ole, kuhani anasema siku za miujiza zimepita. Kwa hivyo hatunazo tena. Kwa njia fulani wanaonekana kusema kwamba Yehova alipoteza nguvu Zake zote."

88 Ndugu, wanajaribu kusema jambo lile lile siku hizi. Lakini Yeye angali ni Yehova Mungu, katika nguvu zile zile, huruma zile zile alizokuwa nazo, na daima atakuwa. Walikuwa nao siku zile ambao waliukana uweza Wake, na wakaikanusha miujiza Yake, wakazikanusha ishara Zake. Nasi bado tungali nao, leo, na tutakuwa nao hata mwisho wa dunia.

89 Tunao wale katika siku hizo ambao waliamini na kupokea. Nasi tunao siku hizi wanaoamini na kupokea. Na kukiwako na kesho, bado watakuwa wakiamini na kupokea.

90 Yesu alisema, "Nitatembea pamoja nanyi, hata mwisho wa ulimwengu." Amina. "Nitakuwa pamoja nanyi, Mwenzenu, Raia mwenzenu pamoja nanyi. Nitatembea pamoja nanyi. Nitawaongozeni katika njia mnazopaswa kupitia, ikiwa tu mtaniruhusu." Napenda hiyo. "Nitakuwa pamoja nanyi hata mwisho wa ulimwengu. Mpaka yote yamekwisha, nitakuwa pamoja nanyi."

91 Angalieni. Ndipo akawaza, "Loo, laiti ningaliishi katika siku ambazo miujiza ilikuwa halisi. Hapa nimepita uwezo wa daktari. Mimi ni mwombaji maskini. Nina familia nyumbani. Labda leo sikupata sarafu yoyote. Watoto wangu wana njaa; na mke wangu, najua ana njaa. Wala sina njia nyingine ya kujikimu. Loo, laiti ningaliweza tu kuona, ningepata kazi katika shamba la ngano mahali fulani. Lakini siwezi kuona."

92 Sasa, ninawazia anapoketi pale, Mungu anaanza kushughulika na moyo wake na kujiandaa kwa ajili ya jambo fulani. Hakujua hata kidogo, pembeni tu kulikuwa na Chemchemi ya Uzima. Haleluya!

93 Hapo pembeni tu, unapoanza kuwazia juu ya uponyaji wa Kiungu, unapoanza kuwazia juu ya Kristo, mweke akilini mwako. "Kukiwapo na sifa yoyote, ukiwemo wema wowote," Biblia ilisema, "yatafakarini hayo."

94 Kama wazo lolote likija, "Vema, labda haingeweza kuwa hivyo. Labda . . ." Liondoe akilini mwako haraka sana. Yatafakari mambo yaliyo mema. Kamwe usiruhusu mawazo

mabaya yapite; ninii tu, ama, usiliache lisimame, kwa vyovyote vile, kama likianza. Dumisha mawazo yako kuwa mazuri: Yesu.

95 Usifikiri, ukiketi hapa kwenye kiti cha magurudumu, wewe, kwamba huna tumaini, hujiwezi. Sivyo ulivyo. Usiruhusu wazo hilo hasi lipite kamwe, au, usiliache likolee. Huwezi kulizuia lisipitie akilini mwako (Hiyo ni kweli.), lakini usiliache lisimame.

96 Kama vile yule mkulima wa kale alivyosema, "Siwezi kuwazuia ndege kuruka juu ya eneo langu." Lakini alikuwa na bunduki ya mitutu miwili, kasema, "Hakika ninaweza kuwazuia kutua." Kwa hiyo fanya jambo lile lile, nawe pia. Unaona? Usiwaache watue. Waache wapite moja kwa moja.

97 Sasa, hii hapa bunduki ya marisau ya kutumia. Agano Jipya na la Kale, ina mitutu miwili. Ni nzuri sana, pia. Nitawaambia, Inawazuia wote.

98 Sawa. Kipofu Bartimayo ameketi hapo na haya yote yakipitia akilini mwake: "Laiti ningalikuwa hapa wakati manabii wakuu waliposhuka barabarani na kushuka kuelekea Yordani. Ningaliwasimamisha kwa dakika chache, kwa mazungumzo mafupi tu, na kuwasihi waniombee. Nami ninaamini Yehova angeyafungua macho yangu."

99 Sasa, kwa ghafla, akasikia kelele. Mnajua, ni ajabu, kwa kawaida wakati Yesu akiwa karibu, kuna kelele kidogo kote. Mnajua, kidogo na—na—napenda hilo; kwa namna fulani kelele kidogo, mnajua. Nanyi mnajua, njia pekee wangeweza kujua Haruni alikuwa hai wakati alipoingia nyuma ya Patakatifu pa patakatifu, kwenye pindo za vazi lake, alikuwa na komamanga na kengele. Na hiyo ndiyo njia pekee wangeweza kujua kama alikuwa hai au la, alikuwa akitoa kelele kidogo mle ndani.

Ninahofia tunahitaji komamanga na kengele tena, naam, kelele ki—kidogo tu.

Na kwa hiyo, kwa kawaida mahali Yesu alipokuwa, kama haikuwa ni mtu fulani anayepiga kelele, ilikuwa ni mtu fulani akimzomea; ilikuwa ni aina fulani ya kelele ikiendelea.

100 Kwa hiyo karibu tu kwenye kona kukatokea kelele. Na muda si muda mwajua mahali hapo pote pakaanza kujaa watu; yule mzee ombaomba ameketi kando ya ukuta. Basi ilionekana kama huko nje kabisa, labda mara mbili ya umbali wa hema hili, hapa, ndipo barabara inaposhukia karibu na Yeriko.

101 Na huko barabarani pengine kulikuwa ndiko ile kelele ilikokuwa. Na kuna watu wanaopita pale na kila . . . Baadhi yao walikuwa wakipiga mayowe, "Mwondoeni, mwondoeni!"

Naye kuhani akipiga kelele, "Mnafiki wee! Hufai chochote."

Na mtu fulani akipiga kelele, "Hosana! Hosana!"

102 Loo, umati uliochanganyikana. Lakini hapo akaja Jemadari mwenyewe wa jeshi la Bwana, ambaye alikuwa amekutana na Yoshua. Amina. Si Yeye ndiye Jemadari wa jeshi? Yeye alikuwa ni Malaika wa Agano, ile Nguzo ya Moto iliyowaongoza wana wa Israeli. Naye Huyu hapa, na hapa tena, akaja, watu walipokuwa wakisema, "Siku za miujiza zimepita, matumaini yote yamekwisha," huyu hapa Jemadari wa jeshi la Bwana, akipita, kwa wakati mzuri kabisa. Sikuzote atawasili vizuri kabisa.

103 Huyu hapa, akipita. Bila shaka yule kipofu, hakujua. Ninaweza kumwazia akiinua kichwa chake huku na huko, aone kama angeweza kusikia vizuri kutoka kwenye sikio hilo. Muda si muda mwajua, mtu fulani akamkanyaga na kadhalika na kumsukuma nyuma. Naweza kumsikia akisema, "Kelele hizo zote ni za nini?" Hakuna aliyemjali; endelea.

104 Walikuwa wakiwasikiliza wengine wakipiga mayowe, "Mwondoeni. Rudini kwenu Nazareti. Hatuhitaji ninii yenu . . . hapa chini katika nchi hii. Rudini"; kelele za kila namna.

Mwingine akipiga kelele, "Yeye ni Bwana wa majeshi. Hosana! Hosana juu zaidi!"

Makutano: Mmoja akipiga mayowe, pengine akimtupia tunda lililooza, na kadhalika.

105 Lakini Yesu, akitembea mbele ya hayo makutano, loo, jamani, uso Wake umeelekea mbinguni. Ni nini kilichokuwa mbele Yake? Akienda moja kwa moja Yerusalemu apate kufa kwa ajili ya dhambi za ulimwengu. Akiwa Yule aliyekuwa, Mwana wa Mungu, Mfalme wa manabii wote, na . . . na akijua ya kwamba hilo lilikuwa mbele Zake, akili Yake, bila shaka, ilikuwa kwenye jambo hilo.

106 Hakuwa akisikiliza makelele ya makutano, "Mwondoeni huyu," na "mwondoeni yule," na "Hosana!" Asingeweza kuusikiliza. Wanafunzi wake wakiwa na wakati mgumu kuzuia ghasia isimfikie: wengine wakijaribu kumgusa wapate kuponywa; wengine walitaka kumpiga kofi au kumpiga na kitu fulani wamwangushe; wanafunzi wakienda, wakawasukumia mbali.

107 Yesu, katika matembezi hayo mazuri, matulivu, thabiti, moja kwa moja barabarani, akienda Zake akiwa ameinua uso Wake kuelekea kwa Baba Yake wa Mbinguni, akitembea kama Mwana mtiifu, vizuri.

108 Na huku akitembea, kila mtu akipiga mayowe, ninaamini ilikuwa ni mwanamke mwema, labda, wakati Bartimayo kipofu aliposema, "Mbona? Kelele hizi zote ni za nini? Nilikuwa nikiwazia tu, hizi kelele zote zinahusu nini?"

Ndipo labda mwanamke mwema aliinama na kusema, "Vema, mwombaji kipofu, Yesu wa Nazareti anapita."

109 Loo, matumaini mapya yaliibuka. Ilikuwa ni nini? Kitu fulani, asingeweza kukiona, lakini alikuwa na hisia nyingine ya kusikia. Kuona sio sikuzote. . . Kuona sio sikuzote kuamini. Wakati mwingine kusikia ni kuamini; imani chanzo chake ni kusikia, si kwa kuona, kwa kusikia. Mtu fulani alimwambia kwamba Yesu wa Nazareti . . .

"Loo, huyo ni Nabii huko juu Ambaye anawaponya wagonjwa?"

110 "Vema, hapana shaka," anasema huyo mama, "baadhi yao wanampigia makelele na kusema, 'Mtoto wangu aliponywa Naye,' nanii . . . mtu mwingine akitembea pale alisema alikuwa kiwete, a—anabeba fimbo ambazo alikuwa akitembea nazo. Lakini kuhani alifikiria . . . "

"Loo," anasema, "msimamishe kwa ajili yangu."

"Ati kumsimamisha? Mbona, usingeweza kumsimamisha. Mwangalie. Anapanda huko barabarani."

111 Halafu basi, yule mzee kipofu mwombaji akasimama kwa miguu yake na kulia, "Ee, Yesu, Ewe Mwana wa Daudi, unihurumie. Ee, Yesu, Ewe Mwana wa Daudi, nihurumie."

112 Sasa, mnajua katika umati huo wote unaoenda bila mpango, ukizungukazunguka, ukihangaika, huku Yesu ameuelekeza uso Wake mbinguni, akienda zake moja kwa moja Kalvari kusulubiwa, huku mizigo ya ulimwengu wote imewekwa begani Mwake, kamwe asingemsikia maskini, mtu huyo mwembamba huko chini nyuma kabisa, kando ya ua huo, ama, kando ya ukuta huo, akipiga kelele, "Unirehemu," huku wakipiga kelele za kila kitu.

Basi alipokuwa akipanda njiani, Bartimayo kipofu akijaribu, alikuwa akisema, "Loo . . . "

Baadhi yao walisema, "Nyamaza. Yuko njiani kule juu."

Yeye . . . Hilo lisingemzuia. Aliinua mkono wake, "Loo, Yesu, Ewe Mwana wa Daudi, unirehemu."

113 Nini kilichotokea? Ilikuwaje? Jambo lile lile lilifanyika kama la yule mwanamke aliyegusa vazi Lake. Alijua hapo ndipo alipopata kumkaribia zaidi. Alijua pengine ndipo atakapowahi kuwa karibu zaidi katika safari ya maisha, hapa, na Yeye. Kwa hiyo jambo pekee aliloweza kufanya ni kuinua imani yote aliyoweza kuamini kwamba Yesu hatampita.

114 Imani yake ilimsimamisha Yesu wa Nazareti akienda Zake Yerusalemu. Kwa ghafla, alipokuwa akitembea, alisimama, akatazama pande zote. Ilikuwa ni kitu gani? Akiwa na Kalvari niani Mwake, na dhambi za ulimwengu mabegani Mwake, pamoja na makutano waliozomea pande zote mbili, maskini ombaomba asiye na elimu, imani ambayo mtu huyo alikuwa nayo ikamsimamisha katika nyendo Zake. Ndipo akageuka, akamtazama, kasema, "Ungefanya nini?"

Kisha akasema, “Bwana, kwamba mimi . . . ”

“Wataka nikufanyie nini?”

Kasema, “Niweze kuona.”

Akasema, “Imani yako imekuponya.”

115 Ninaweza kumwona anapogeuka, akipanda njiani; maskini Bartimayo kipofu amesimama pale, akisema, “Aliniambia nimepona?” Mwangalieni akijaribu kuuangalia mkono wake. Kasema . . .

Loo, ninaweza kusikia baadhi yao wakisema, “Hakuna tofauti kwako. Wewe—wewe si—wewe si tofauti.”

116 “Lakini, lakini, lakini Yeye aliniambia. Aliniambia mimi . . . ” Baada ya kitambo kidogo yeye . . . nuru ya mchana ikaanza kumpambazukia. Muda si muda mwajua, angeweza kuiona mikono yake. Huyu hapa anapanda barabarani, akipiga mayowe, na kupaza sauti, na kumsifu Bwana. Imani yake ilikuwa imemponya. Imani yake ilikuwa kubwa sana mpaka ikamsimamisha Yesu wa Nazareti na ku—kuongea Naye.

117 Na kama mwombaji kipofu, asiye angalau hata na nguo za kutosha, hata, kuificha ngozi yake angeweza kusimamisha . . . nanii, labda, mtu ambaye hata asingeweza kuandika jina lake mwenyewe, kama imani yake ingeweza kumsimamisha Yesu wa Nazareti katika makutano ya watu walioililia Damu Yake, akiwa na mzigo moyoni Mwake, na kujua kwamba mauti yalikuwa mbele Zake pale Kalvari, ni zaidi sana vipi imani yako inapaswa kumsimamisha, usiku wa leo, na kumleta kwa mahitaji yako binafsi. Haleluya!

118 Loo, jamani. Nilikuwa nikisoma hadithi ndogo juu yake muda si mrefu uliopita. Labda nina dakika moja tu au mbili kwa ajili yake. Walisema kwamba alikuwa na msichana mdogo. Hajawahi kumwona. Naye sikuzote aliomba kwamba angemwona msichana huyo mdogo.

119 Nao wananiambia ya kwamba Bartimayo kipofu alikuwa na ba—baadhi ya hua wadogo ambao walifanya vitimbi vichache. Ingembidi kufanya jambo fulani kuvutia usikivu wa watu, wapita njia. Kulikuwa na ombaomba wengi sana, wasingeweza kupata cho—chochote hata kidogo. Lakini kama wangeweza kuwafanya hawa njiwa wadogo kufanya vitimbi vichache mmoja juu ya mwingine ambapo . . . (Sasa, huenda hiyo hadithi ikawa ni ya kujibunia.) . . . kufanya vitimbi mmoja juu ya mwingine, mbona, ingewasimamisha watu na wangewatazama hao njiwa wadogo, ndipo wangewazia, “Loo, vema, mpe sarafu.” Mnaona? Na hivyo ndivyo alivyopata, riziki yake.

120 Na kwa hiyo walisema mkewe aliugua usiku mmoja, naye akatoka na kuomba, ndipo akasema, “Mungu, sina chochote. Mimi ni ombaomba maskini. Lakini kama utamjalia tu mke wangu apone, ni—nitakupa hawa njiwa wawili kesho kama

dhabihu." Kwa hiyo mke wake akapona, naye akatimiza ahadi yake.

121 Kasema muda si mrefu baada ya hayo kwamba msichana wake mdogo aliugua, mahututi kabisa, karibu na kufa. Basi ilisemekana yule ombaomba kipofu alilia karibu usiku kucha. Ikasemekana alitoka nje akaomba, akasema, "Bwana, sina chochote kingine cha kukupa."

122 Lakini siku hizi, tuna mbwa, mwajua, wanaowaongoza vipofu. Wanasema walikuwa na mwana-kondoo wakati huo, kwamba wangemfunga mwana-kondoo na kumfundisha kuwaongoza vipofu.

123 Akasema, "Bwana, ni—nina kitu kimoja tu kilichosalia, nacho ni mwana-kondoo wangu, lakini iwapo—iwapo utamponya tu msichana wangu mdogo, na usimwache afe... Sijawahi kumwona. Kama utamjalia tu msichana wangu mdogo kuishi, na—nakuahidi nitakupa mwana-kondoo wangu kesho kama dhabihu."

"Mbona," akasema, "Bwana akamponya msichana wake mdogo."

124 Kesho yake akienda zake kumpeleka mwana-kondoo kwenye dhabihu, mpaka hekaluni akamtoe kafara, kasema, kuhani mkuu Kayafa alikuwa amesimama ukutani, naye akasema, "Bartimayo kipofu, unaenda wapi?"

125 Akasema, "Loo, kuhani mkuu, hiyo ni sauti yako?" Akasema, "Ninaenda hekaluni kumtoa dhabihu huyu mwana-kondoo. Mungu alimponya msichana wangu mdogo, nami nikamwahidi ningempa mwana-kondoo huyu."

126 Naye akasema, kuhani mkuu akasema, "Loo, Bartimayo kipofu, huwezi kumtoa kafara huyo mwana-kondoo. Hima, nitakupa pesa uende ukanunue mwana-kondoo kule juu sokoni ukamtoe kafara *huyo* mwana-kondoo."

Akasema, "Loo, kuhani mkuu, kamwe sikumwahidi Mungu mwana-kondoo *yeyote*; nilimwahidi Mwana-kondoo *huyu*."

127 Akasema, "Lakini, kipofu Bartimayo, huwezi kumtoa huyo mwana-kondoo. Mwana-kondoo huyo ndiye macho yako. Huyo tu ndiye macho uliyo nayo, kipofu Bartimayo. Huwezi kumtoa mwana-kondoo huyo. Ndiye macho yako."

Akasema, "Loo, kuhani mkuu, nitatimiza ahadi yangu kwa Mungu, naye Mungu atatoa Mwana-Kondoo kwa ajili ya Bartimayo kipofu."

128 Ilikuwa ni siku yenye baridi. Lakini kelele hizo zilipofika kando ya hilo jengo, Mungu alikuwa amemtoa Mwana-Kondoo kwa ajili ya macho ya Bartimayo kipofu.

129 Rafiki yangu mpendwa, Mwana-kondoo yuyo huyo ametolewa kwa ajili yako usiku wa leo. Kama wewe ni mwenye

dhambi, na macho yako hayajawahi kufunguliwa kuiona Nuru ya Mungu kama mwanamume, ama mwanamke, mvulana, au msichana aliyeokoka, Mwana-Kondoo huyo ametolewa dhabihu kwa ajili yako usiku wa leo. Ikiwa wewe ni mgonjwa na uko karibu kufa, na daktari wako amefanya yote anayoweza kufanya, mtu huyo amefanya awezalo, lakini kuna Mwana-Kondoo kwa ajili ya ugonjwa wako usiku wa leo.

Na tuinamishe vichwa vyetu tunapozungumza na Mwana-Kondoo huyu.

130 Ee, Mungu, tunafundishwa katika Biblia ya kwamba juu ya kiti cha enzi katika nchi ya Utukufu kulikuwa na Mmoja aliyeketi Ambaye alikuwa na Kitabu kilichotiwa muhuri upande wa nyuma kwa Mihuri Saba. Naye huyo nabii akalia kwa sababu hapakuwapo na mtu yeyote aliyestahili kukitwaa kile Kitabu kuifungua ile Mihuri. Ndipo akatokea Mwana-Kondoo, Yule aliyechinjwa tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu. Naye alistahili kukitwaa kile Kitabu na kuifungua ile Mihuri, huyo Mwana-Kondoo wa Mungu.

131 Ninaweza tu kuwazia, wakati kipofu Bartimayo alipojua ya kwamba alikuwa amesimama, kwa namna fulani, au, alipoingia Mbele za Mwana-Kondoo Wake aliyetolewa: Tunamwona sasa, sio akijaribu kukunja kanzu yake na kuilaza chini vizuri, ili kwamba, hata kama macho yake hayatafunguliwa, mbona, ataweza kuipata. Tunafundishwa kwamba alitupilia mbali vazi lake. Alijua angelipata, maadamu alifika kwa huyo Mwana-Kondoo.

132 Loo, njoo, Mwana-Kondoo wa Mungu. Ondoa upofu kutoka kwenye macho ya watu, usiku wa leo, wanaotumaini kwa sababu wamejiunga na kanisa au kitu fulani cha kimwili kilichotokea. Mungu, jalia upendo wa Mungu umiminike moyoni mwao. Tujalie, Bwana. Ondolea mbali hali zote za mawe na uache upendo wa Kiungu umiminike moyoni mwao kwa Mwana-Kondoo huyo, usiku wa leo. Na uwaponye wagonjwa. Kwa kuwa tunaomba katika Jina Lake.

133 Na wakati tumeviinamisha vichwa vyetu, sijui kama kuna mmoja hapa, usiku wa leo, ambaye huenda ikawa anapapasa-papasa katika giza la kanisa, bila kujua ageukie upande gani, kama atakuwa Mmethodisti, ama abaki Mpresbiteri, au Mpentekoste, ama hujui tu la kufanya? Je, hutaki Yeye ayafumbue macho yako ya kiroho usiku wa leo kwa kukubariki na kuyaondolea mbali mashaka yote?

134 Ikiwa wewe ni mwenye dhambi, hapa, na unataka kukumbukwa katika maombi, inua tu mkono wako kwa Mungu wakati kila mtu anaomba sasa. Nami nitawaombea ninyi, na hao wengine, kusanyiko pia litafanya hivyo. Je, utainua mkono wako, mtu fulani anayemhitaji Kristo usiku wa leo na unajua ya kwamba unamhitaji Kristo? Je, utainua mkono wako? Siujui

moyo wako; Mungu anaujua. Lakini Mwana-kondoo aliyepitia Yeriko siku ile . . .

135 Mungu akubariki, huko nyuma, ndugu yangu mpendwa. Mungu akubariki, naam, na wewe, dada yangu. Mtu mwingine utainua mkono wako? Hiyo ni . . . Mungu akubariki, dada yangu. Nakuona huko nyuma. Na Mungu akubariki, ndugu yangu, unayeketi karibu na nguzo, hapo. Mungu akubariki upande wangu wa kushoto hapa, naam, unayeketi karibu na nguzo hapo, tena, mtu mwingine.

136 "Yesu, Ewe Mwana wa Daudi, unirehemu. Mungu, najua ni—ninaweza . . . huu unaweza kuwa ndio usiku wangu wa mwisho duniani. Sina budi kukutana na Wewe. Nimelipuuza. Kwa kweli sina uhakika juu ya wokovu wa nafsi yangu. Nataka unikumbuke, Mungu, sasa hivi, kwamba katika mkutano huu na—nataka uniokoe, usiku wa leo, na kwa kweli uurekebishe moyo wangu, ili kwamba mauti yakinipiga, nami nihisi mapigo yangu ya moyo yakinivizia, nami nibonyeze mto wa kufa, daktari aondoke mlangoni, na kusema, 'Hakuna la zaidi linaloweza kufanywa, huyo mwanamume ametuacha,' au, 'huyo mwanamke ametuacha,' wapendwa wangu watoke chumbani wakilia, mivuke baridi ya mauti inaelea kupitia chumbani, Mungu, nataka kukuona ukiliangazia bonde la uvuli wa mauti. Nakutaka uyarekebishe sasa."

137 Je, utainua mkono wako, mtu ambaye hajainua mkono wake? Mungu akubariki, ndugu yangu. Naam, bwana, amina, ndugu.

138 Unajua, miaka ishirini na mitatu iliyopita, nilisuluhisha hilo. Nimekuwa na furaha tangu wakati huo. Nilimwambia Bwana si—sikutaka matatizo yoyote pale mtoni. Kila siku ninajifanyia hesabu. Sitaki matatizo yoyote.

139 Itakuwa mbaya sana asubuhi hiyo: mayowe yote na vilio vyote ulivyowahi kusikia; matajiri wakitupa pesa zao mitaani; pinde za mvua zikimemetesha angani; radi ikimulika; ngurumo zikinguruma; mwezi ukigeuka kuwa damu, na kudondoka kama damu nyeusi ikianguka; jua likikataa kuangaza; miamba ikinguruma; atomi zikilipuka kila mahali; moto ukishuka. Huh-uh. Sitaki tatizo wakati huo. Nataka kuwa na uhakika nalo. Ninataka kuhakikisha sasa hivi, maana, mnajua, hii inaweza kuwa ndiyo saa ya mwisho nitakayokuwa hapa, ama wewe, mojawapo. Yote yamekwisha basi. Jinsi mti unavyoegemea, ndivyo unavyoanguka.

140 Je, kunaweza kuwa na mwingine, kabla tu hatujafunga sasa na kufanya maombi? Unajua, Mungu anaujua moyo wako. Usitegemee theolojia. Usitegemee maarifa ya kichwa. Kama hujapata ujuzi wa kweli na Mungu, na kujua ya kwamba umepita toka mautini kuingia Uzimani, huo upendo wa Kiungu wa Mungu unatawala moyoni mwako, usibahatishe juu yake,

rafiki. Kumbuka, ninawaambia katika Jina la Bwana, hakuna kitu kingine kitakachofanya kazi.

Loo, unasema, “Ninahubiri Injili.” Hiyo haijalishi. “Nimetoa pepo. Nimekuwa na huduma za uponyaji.” Hiyo haijalishi.

141 Yesu alisema, “Wengi watakuja Kwangu siku hiyo, ‘Bwana, hivi sikuhubiri katika Jina Lako, nikatabiri? Hivi mimi, kwa Jina Lako, sikutoa pepo na kufanya miujiza mingi?’” Atasema, “Ondokeni kwangu, enyi watenda maovu. Hata sikuwajua.”

Afadhali uwe na uhakika. Kabla tu hatujaomba, mara nyingine tena, mikono yoyote ambayo bado haijainuliwa, waweza kuinua mkono wako kwa ajili ya maombi?

Vema. Twaweza...? Mungu akubariki, mama, Mungu akubariki. Nauona mkono wako. Hiyo ni kweli. Tufanye tu maombi sasa.

142 Baba wa Mbinguni mwenye fadhili, kulikuwako na vijana kwa wazee, wote wawili, walioinua mikono yao. Njoo sasa, sivyo, Yesu? Nena tu amani kwenye kilindi cha moyo wao. Hawangeweza kuinua mikono yao pasipo Wewe kuwaambia; lakini walifanya hivyo. Nawe umesema katika Neno Lako, “Yeye alisikiaye Neno Langu, na kumwamini Yeye aliyenipeleka, yuna uzima wa milele, wala hataingia hukumuni; bali amepita kutoka mautini kuingia Uzimani.”

143 Tunajua kwamba sasa hivi mabadiliko ya vivuli vyeusi vya mauti vilivyoning’inia usoni mwa watu hawa sasa vinarudi nyuma, na matumaini yanakuja, sio kwa jicho la kimwili, bali katika jicho la kiroho, ya kwamba wamefanya lililo sahihi na wamemkubali Kristo, sasa, kama Mwokozi wao. Mungu, naomba ya kwamba giza lao lote litakimbia, na nguvu za mjaribu, za mwenye shaka zitavunjwa, nao wataishi katika maisha ya Kikristo na Nuru siku zao zote zilizosalia, kisha waje Nyumbani Kwako kwa amani katika wakati wa mwisho.

144 Mungu, jalia kwamba katika ulimwengu mwingine, kwamba usiku fulani, siku fulani, hasa, kwa kuwa hakutakuwako na usiku, kwamba nitakutana nao, kama si hapa duniani, tuketi chini kule kwenye ule Ufalme, ambako Moody, na Sankey, Finney, Knox, Calvin, Paulo, Petro, Yakobo, Yohana, ambako wengi wa marafiki zetu hapa, Paul Rader, mpendwa Ndugu Upshaw, wengi wa wale askari wengine hodari, wa kale, ambao wamepita ng’ambo ya pazia, wamepita tu ng’ambo ya pazia, wa—wanaelewa, naomba nikutane na hao wote, pamoja na hawa usiku wa leo ambao wamekukubali Wewe.

Hadi wakati huo, Baba, wadumishe watamu na wenye furaha katika ujuzi wao na Wewe, kwa kuwa tunaomba katika Jina la Yesu. Amina.

Laiti ningaliweza kuimba. Wimbo ule mzuri . . . ? . . . [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] " . . . ndipo usiku wote ukageuka kuwa mchana."

145 Ni wangapi wanaompenda kwa upendo halisi wa Kiungu? Sasa, mnajuaje hilo? Huyu hapa shahidi mmoja: kwa sababu mnapendana. Hiyo ni kweli. Tunajua tumepita toka mautini kuingia Uzimani tunapowapenda ndugu zetu. Yesu alisema, "Hivyo watu wote watatambua ya kuwa ninyi mmekuwa wanafunzi wangu, mkiwa . . . " Unapokuwa mshiriki wa kanisa? Hapana, hapana. Uh-uh. Unapopiga kelele? Hapana, hapana. Unaponena kwa lugha? Hapana, hapana. Unapokuwa na ibada ya uponyaji, kuhubiri Injili? Hapana, hapana. "Mkiwa na upendo ninyi kwa ninyi."

146 Marafiki, mimi sio mvulana mdogo tena. Nimeona majaribio mengi, bali bado sijawahi kuona chochote ambacho kinaweza kushinda upendo. Huondoa tu kila kitu njiani. Upendo hushinda mnyama mwitu. Upendo hushinda. Ndio nguvu tu zinazoshinda zaidi zilizopo, kwa sababu ni Mungu.

147 Mnajua ni kwa nini naweza kuwasaidia? Ni kwa sababu mnanipenda na mnaniamini. Kama hamngeniamini, haijalishi ni matendo ya aina gani Mungu angetenda kupitia kwangu, mngali hamngepata faida yoyote. Mnajua hilo? Hayo ndiyo mafanikio yangu na Bwana: watu wananipenda nami nawapenda. Na hapo ndipo mafanikio yanapotokea. Vinginevyo, isingalikuwa . . .

148 Mwangalieni Yesu. Yeye alisema, "Nisipozitenda kazi za Baba Yangu, msiniamini Mimi. Lakini nikizitenda kazi za Baba Yangu, basi aminini kwa sababu ya hizo kazi." Mnaona?

149 Sasa, kuna mwanamke aliyegusa vazi Lake, akaponywa. Kipofu mmoja alimpigia makelele akaponywa. Lakini kulikuwa na askari wa Kirumi ambaye hakuamini kwamba Yeye alikuwa Nabii, na kundi la Wayahudi ambalo halikuamini. Wakaweka kitambaa usoni Mwake, wakampiga kwenye utosi wa kichwa, wakasema, "Sasa, wewe mtabiri, twambie ni nani aliyekupiga. Ikiwa unajua mambo haya yote, twambie ni nani aliyekupiga nasi tutakuamini ikiwa utatwambia sasa." Hakufungua kinywa Chake kamwe.

150 Hapana, kazi za Mungu hazipaswi kufanywa mzaha. Yesu kamwe hakuja kufanya mizaha, wakati ule; Yeye haji kufanya mizaha, sasa. Shetani alijaribu kumjaribu, kasema, "Fanya mwujiza. Hebu nikuone ukiufanya."

Hivi hamjawasikia watu wakisema hivyo? "Hebu nikuone ukifanya jambo fulani. Hebu nikuone."

151 Mtu mmoja, si muda mrefu uliopita, bila kujua, ndugu mmoja, nilipokuwa nikihubiri huko Arkansas, kasema, "Nitaninii, kwa ushahidi mmoja wa kimwili kwamba mtu mmoja aliwahi kuponywa, uponyaji wa Kiungu, tutalipa dola elfu moja, kanisa letu."

152 Kwa hiyo, nilienda tu na kuwachukua madaktari kadhaa na takriban visa vinne vya kansa vilivyokuwa vimeponywa, daktari alisema hivyo, nikavipeleka nyumbani kwake. Nikasema, "Tutatuma tu hizo kwenye misheni za kigeni."

Nilipofika mlangoni, "Loo," akasema, "wewe ni Mchungaji Branham?"

Nikasema, "Ni mimi."

153 Akasema, "Vema sasa, inabidi uende hapa Texas mahali fulani, nasi tutamchukua msichana mdogo, nami nataka uingie miongoni mwa ndugu zangu," kasema, "Sina hizo pesa."

154 Nikasema, "Hapana, nimekuja kuzichukua. Hawa hapa watu ambao madaktari waliwakatia tamaa na kusema walikuwa na kansa, nasi tukawaombea, na Yesu akawaponya. Sasa, ulisema kwenye redio kwamba hizo ndizo ungetoa. Sasa, hebu tuzipate."

155 Nikasema, "Huyu hapa mmoja wao, alikuwa nesi wa Mayos, mmoja wa Ma-. . .Daktari Mayo, kutoka kwenye Kliniki ya Mayo, mmoja wa wauguzi wao. Tunataka kuchukua hizo dola elfu moja."

156 Akasema, "Vema sasa, tutaenda huku, nasi tutamchukua m—mtu, msichana mdogo, nami nitakata mkono wake kwa kisu, ndipo nawe uushikilie mbele ya ndugu zangu, na kuuponya, ndipo basi tutaamini."

157 Nikasema, "Ndugu, wewe ndiye unahitaji uponyaji kutokana na kupungukiwa akili." Nikasema, "Hiyo—hiyo kweli ni. . . " Nikasema, "Mtu yeyote ambaye angewazia hilo, kuna kasoro *hapa* juu." Mnaona? Hiyo ni. . .Nikasema, "Ni roho ile ile ya kale iliyosema, 'Shuka utoke msalabani nasi tutakuamini.'"

Roho yule yule wa kale aliyesema, "Fanya mwujiza hapa mbele yangu, nasi tutakuamini."

158 Nikasema, "Ndugu, wewe ni. . .naomba kwamba Mungu. . . Ninakupenda, na huo si wa kinafiki." Nikasema, "Lakini ninakupenda, nami ninaomba kwamba siku moja Mungu atairehemu nafsi yako yenye dhambi."

Kasema, "Sifanyi dhambi."

Nikasema, "Dhambi ni nini? *Dhambi* ni 'kutokuamini.'" Hiyo ndiyo dhambi pekee iliyopo, ni kutokuamini. Nikasema, "Bila shaka ni dhambi."

159 Sasa, na tusiwe wenye dhambi, wasioamini, usiku wa leo, lakini hebu tuitupe imani yetu pamoja na kuamini kwa moyo wetu wote. Mtafanya hivyo tunapoomba kwa dakika kumi na tano au ishirini zijazo? Vema.

160 (Wangali wanasambaza za A? Loo.) Za F, sambazeni kadi za maombi za F. Nilifikiri, siku kadhaa, zilikuwa mia kadhaa.

Vema, tunabadilisha usiku wa leo kuwa kadi za maombi F basi. (Ulisambaza ngapi? Mia moja?) F mia moja. Hebu tuanzie kutoka—hebu tuanzie kutoka ishirini usiku wa leo. Ni nani aliye na F, ishirini? Angalieni iwapo niko . . . Wote . . . F, ishirini? Ishirini na moja? Ni nani aliye na F, ishirini na moja? Inua mkono wako. Angalia kama tuko sawa sasa.

Angalia kadi ya jirani yako. Wanaweza kuwa ni viziwi, bubu labda. Angalieni kadi hizi kwenye vitanda, na kadhalika.

Nawe una kadi ya maombi, mama? Naam, sawa. Una kadi ya maombi hapo? Vema.

161 F, ishirini na moja, ishirini na mbili, ishirini na tatu, ishirini na nne, ishirini na tano, ishirini na sita, ishirini na saba, ishirini na nane, ishirini na tisa, thelathini. Sasa, acha wapange mstari kwanza, papa hapa. Vema.

162 Vema, wakati wanapokuja . . . Sasa, angalieni pande zote. Ikiwa ni mtu yeyote ambaye hawezi kusimama, vema, i—inua tu mkono wako nasi tutakuwa na mabawabu wa kukuleta hapa. Unaona?

163 Vema, sasa, hizo ni, nafikiri, ishirini hadi thelathini. Sasa, thelathini na moja, thelathini na mbili, thelathini na tatu, thelathini na nne, thelathini na tano, hebu wafuate sasa. Vema, hiyo itakuwa ishirini hadi thelathini na tano. Sasa, hebu wasimame kwanza, sasa: F, ishirini hadi F, thelathini na tano. Sasa, tuone jinsi watakavyojipanga. Labda tunaweza kuwaleta wengi zaidi na tupate kujua sasa.

164 Sasa, nataka usikivu wenu mkamilifu sasa kwa dakika chache zijazo. Sasa sikiliza, rafiki mpendwa, huu ni mkutano wako. Sasa, mimi, usiku wa leo, nikizungumza juu ya jambo hili, baada ya kueleza ibada za uponyaji . . .

165 Sasa kumbukeni, siamini ya kwamba kuna nguvu zozote katika mwanadamu za kuponya mtu. Siamini kwamba kuna nguvu zozote ambazo mtu yeyote anazo za kumponya mtu. Ninaamini kwamba mambo mawili hayawezi kufanywa: kwamba hakuna mtu anayeweza kusamehe dhambi wala kuponya ugonjwa. Kumbukeni hilo. Hakuna awezaye kufanya hivyo, kwa sababu Yesu amekwisha kufanya hivyo pale Kalvari, nawe unaukubali kama imani yako binafsi katika kazi Zake zilizokamilika. Je, mnaamini hivyo? Semeni, "Amina." [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Mnaona? Ninyi . . .

166 Sasa Mungu ameweka baadhi ya ishara kanisani. Kwanza, mhubiri; hiyo ndiyo ishara iliyo bora zaidi, kuhubiri Neno. Kama ingekuwa ni mimi, kama usingelikubali neno langu kwa ajili yake, hilo lingelitatua, lakini si Baba yetu. Kisha, Yeye huwaweka wengine kanisani. Baada ya wahubiri, anaweka waalimu, anaweka manabii, anaweka karama za uponyaji. Hiyo haimaanishi kuponya sasa; hiyo inamaanisha imani katika uponyaji. Mnaona?

Ni kama tu kuhubiri, vivyo hivyo. Sio nguvu za kuponya. Unapodai una nguvu za kuponya, basi unaziondoa Kalvari.

167 Ninaamini kama ukidai hilo, ndugu, kwa ninii yangu... Ikiwa nimekosea, mnisamehe. Lakini jinsi ninavyoyaona Maandiko, ni kwamba tayari imekamilika. Ingewezekanaje...?

168 Ndu—ndugu katika Wafanyibiashara Wakristo alinunua na kunipa suti hii. Ililipiwa. Alinipa yapata mwaka mmoja uliopita, kabla sijaenda ng'ambo. Kasema, "Billy, unahitaji suti." Yangu ilikuwa imechakaa kabisa kwenye kola. Ndipo akanunua na kunipa suti hii.

169 Sasa, hakuna haja ya mtu yeyote kujaribu kuilipia. Tayari imelipiwa. Ni yangu kwa zawadi, sivyo? Na hivyo ndivyo wokovu ulivyo, na hivyo ndivyo uponyaji ulivyo. "Alijeruhiwa kwa makosa yetu; kwa kupigwa Kwake sisi tuliponywa." Hiyo ni kweli?

170 Sasa, ni wangapi...? (Wote wako huku? Naam? Kila mtu yupo? Sawa, mnataka wengine zaidi, ama hao...?) Naam, haijalishi ni wangapi wanaosimama. Sisi...Hilo silo wazo lake. Jambo ni kwamba, rafiki, ni kumfanya Roho Mtakatifu atembee kati ya watu.

171 Sasa, angalieni, huyu hapa mwanamke amesimama hapa. Hii ni karama ya Kiungu. Na ni, huyu hapa mama amesimama hapa mbele yangu. Yeye ni mgeni kabisa kwangu. Sijawahi kumwona maishani mwangu. Hivi hatufamiani, dada, mmoja kwa mwingine? Hakika hatufahamiani.

172 Sasa, jiweke mwenyewe hapa. Sasa, kwanza ninaweza kukwambia kwa Biblia, hilo ni Neno la Milele la Mungu, na hilo ni Kweli. Na chochote ambacho ni kinyume na Hicho si cha Mungu, nionavyo mimi. Haina budi kuwa Hili; Hili ndilo msingi. Hilo ni Neno la Mungu, kwanza.

173 Vema, halafu, pili, anao wahubiri wanaoshuka na kulihubiri Neno hili, ambao wanalielewa, na kuwaambia watu. Halafu, tena, Yeye anawaweka manabii kanisani. Manabii ni waonaji wanaoona mambo awali, na kusema mambo yanayotokea. Na yote ni kwa Roho wa Mungu.

174 Basi Yesu alipokuwa hapa duniani, kwa wageni, Yeye kamwe hakudai kuwa mponyaji. Ni wangapi wanaojua jambo hilo? Inua mkono wako. Yeye alisema, "Mimi siye mponyaji." Alisema, "Mi—Mimi...Si Mimi nizitendaye hizi kazi. Ni Baba Yangu aishiye ndani Yangu. Yeye huzitenda hizo kazi." Je, hiyo ni kweli?

175 Naye Yesu akasema, "Amin, amin..." Yohana Mtakatifu 5:19, "Amin, amin, nawaambia, Mwana," (ule mwili) "Siwezi kufanya neno lolote," (Mwana, Roho Wake) "Siwezi kufanya neno Mwenyewe, ila lile ambalo Baba aliye ndani Yangu ananionyesha." Mnaona? "Na yale Baba anayonionyesha kwa ono, hayo ninaenda kutenda." Je, hivyo ndivyo alivyosema?

176 "Amin, amin, nawaambia, Mwana hawezi kutenda neno Mwenyewe, ila lile amwonalo Baba akilitenda, ndilo Mwana atendalo vile vile"; alipoulizwa kuhusu kutowaponya wote kule Bethesda, alimponya tu mtu mmoja aliyelala juu ya godoro.

177 Tazama hapo. Naye Yesu alijua mtu huyu alikuwa pale, na alikuwa amekaa pale, na kwa muda mrefu katika hali hii. Je, hiyo ni kweli? Ni wangapi wanajua Maandiko yanasema hivyo? Yesu alijua alikuwa huko—alikuwa huko . . . Hakika, Yeye alijuaje jambo hilo? Baba alimwonyesha.

178 Hapo waliketi viwete, na vipofu, na waliopindika, na vilema, na viwete, Yesu akiwazunguka moja kwa moja mpaka akampata mtu yule ambaye Mungu alikuwa amemwonyesha. Huyo hapo. Kasema, "Je, unataka kuwa mzima, bwana?"

Akasema, "Sina wa kuniweka majini." Kasema, "Mtu hunitangulia mle."

Kasema, "Litwae godoro lako uende zako nyumbani."

179 Hakuhoji hata kidogo. Alilitwaa tu godoro lake, akaliweka mabegani mwake, akaanza, nguvu zikaanza kumjia, naye huyo akaenda zake. Yesu akaondoka na kuwaacha hao wengine, maana Baba hakuwa amemwonyesha wengine. Mnaona?

180 Yule mwanamke kisimani . . . Hili hapa tena, kuanza na mwanamke usiku wa leo. Sasa angalieni, yeye ni mwanamke, mimi, mwanamume. Sasa, hatujawahi kukutana maishani mwetu. Sasa hebu tuone kama haya ni Maandiko.

181 Sasa, Yesu alipanda na kuketi kisimani. Baba alikuwa amemtuma kisimani. Hakujua. Hayo tu ndiyo aliyojua: Panda uende kisimani, juu, huko Samaria.

Sasa, Baba, Mungu . . . Je, huamini kwamba Yeye anafanya kazi ndani yetu? Je, Yeye hakusema angefanya hivyo? "Mambo yale yale ninayofanya Mimi, ninyi nanyi mtayafanya."

Anaenda kule na kuketi kisimani. Vema, hivyo ndivyo Baba alivyomwambia afanye.

182 Baba alinituma kwenye Bonde la San Fernando, California, katika mkutano huu wa hema. Nilikuja tu hapa. Hayo ndiyo yote ninayojua. Niko hapa tu. Yule pale mwanamke amesimama.

Basi, mwanamke akaja kuteka maji, kwa hiyo Yesu akaendelea kuzungumza naye. Akasema, "Nipe maji ninywe."

Akasema, "Si desturi kwenu Wayahudi kuwaomba Wasamaria kitu kama hicho, hatuna uhusiano."

183 Walipokuwa wakiendelea na mazungumzo, waliendelea kuzungumza, mpaka Yesu akapata mahali hasa ambapo shida yake ilikuwa. Akasema, "Nenda, kamwite mumeo."

Akasema, "Sina yeyote."

Kasema, "Hiyo ni kweli. Unao watano."

184 Akasema, "Naona ya kuwa Wewe ni Nabii." Akasema, "Sasa, tunajua, sisi Wasamaria, tunajua ya kwamba ajapo Masihi, Yeye atatwambia mambo yote." Lakini hakuweza kuelewa Yeye alikuwa ni Nani. Kasema, "Hapana shaka Wewe ni Nabii."

185 Yesu akamwambia kwamba Yeye alikuwa ndiye Masihi. Je, hiyo ni kweli? Naye alipofanya hivyo, alikimbilia mjini na kuwaambia hao watu, kasema, "Njoni hapa mumwone Mtu. Nilikuwa nimesimama huko nje, nilitoka tu kwenda kuteka maji, ndipo huyo Mtu akaniambia uovu ninaofanya," au njia yoyote aliyolielezea. Kasema, "Haimkini kuwa huyo ndiye Kristo? Je, hiyo siyo ishara ambayo Kristo alikuwa awe?"

186 Sasa, lile kanisa kubwa siku hizo liliwazia nini juu Yake? Walisema Yeye alikuwa ni nani? "Beelzebuli, ibilisi, mkuu wa wapiga ramli wote na kila kitu kilicho kiovu."

Lakini alisema Yeye alikuwa ni nini? "Masihi." Alijua hiyo ilikuwa ndiyo ishara ya Masihi.

Na kama Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele, ingali ni ishara ya Masihi. Hiyo ni kweli.

187 Kwa hivyo, sio mimi, mimi ni mwanadamu tu, ambaye... Na wewe ni mwanamume tu, wanawake. Yeye ni mwanamke tu; mimi mwanaume. Lakini Masihi, Yesu aliyefufuka, Yule aliyesema, "Mambo haya ambayo mimi... Bado kitambo kidogo na ulimwengu hautaniona tena (wasioamini), lakini ninyi mtaniona Mimi, kwa maana nitakuwa pamoja nanyi hadi mwisho wa dunia. Na mambo yale yale nifanyayo Mimi, ninyi nanyi mtayafanya." Ati nini? Kadiri Baba anavyoonyesha, naigiza tu katika mchezo wa kuigiza.

Sasa, kama nilivyoeleza jana usiku jinsi ambavyo maono kama haya ni ya ziada. Ono kuu ni wakati anapojitambulisha Mwenyewe. Lakini haya ni ya ziada.

188 Sasa, nitawaombeni ninyi nyote, tafadhalini, mwe na kicho kabisa nami nitatoa pendekezo kwenu. Nitaiangalia mstari, kwanza. Siamini... Ninyi watu wote, hakuna hata mmoja wenu anayenifahamu, sivyo? Kuninii tu, mimi, kufahamiana nami... Inua mkono wako endapo hatufahamiani, ninyi nyote kwenye mstari wa maombi hapo, inueni mikono yenu kama sisi sote hatufahamiani. Vema.

189 Ni wangapi huko nje wasio na kadi za maombi, na hata hivyo mnataka kuponywa, nasi hatufahamiani? Hebu tuone mikono yenu ikiinuliwa, popote.

190 Vema, aminini tu. Sasa kumbukeni, yule kipofu Bartimayo ambaye angeweza kuvuta imani kupitia kwa Bwana Yesu; yule mwanamke aligusa vazi Lake.

Sasa kama Yesu atakuja na kutekeleza papa hapa, ambapo papa hapa, dhahiri mbele yenu ambalo ninalitangaza...

191 Na kama mtu fulani angetaka kuchukua mahali pangu na kuja hapa, umekaribishwa kwenye maikrofoni. Vema, shuka kwenye mstari wa maombi. Kama hufikiri kuwa ni ya kweli na ya Mungu, vema, njoo uchukue maikrofoni. Umekaribishwa.

192 Sasa, lakini, hapa, kama ndivyo, nami nasema Kweli, nami ninasema kweli juu ya Kristo, basi kama nikizungumza juu Yake na kusema ukweli, Yeye anawajibika kujibu na kusema kwamba nilisema ukweli.

193 Basi, mna haki ya kunitilia shaka, sasa. Lakini kama Yeye akifanya yale niliyosema atafanya, ya kwamba amefufuka katika wafu na anafanya vile vile, basi usipoamini basi, basi Mungu airehemu nafsi yako yenye dhambi. Hayo ndiyo yote ni—ningejua.

194 Sasa, kama Yesu atafanya jambo lile lile kwa mwanamke huyu hapa, yeye akijua ya kwamba hatujawahi kukutana maishani, kama Yeye atafanya, na kujua kilichomleta hapa, kama vile Yeye alivyojua huyo mwanamke alivyokuwa, kule juu, kuhusu, je, kila mmoja wenu, kwa nia moja na moyo mmoja, atamwamini Bwana Yesu Kristo, na kuamini ya kwamba Yeye atakupa usiku wa leo, kile hasa kilichokuleta? U—utafanya hivyo? Inua mkono wako. Laiti kila mmoja wenu ambaye anaamini kweli ungeinua mkono wako. Anakutazama. Amina. Mungu akubariki.

195 Sasa, Baba wa Mbinguni, si—sijui la kufanya zaidi kwa maarifa yote niliyo na—nayo, wala sina yoyote ila yale yatokayo Kwako. Nami naomba, Baba, ya kwamba Wewe sasa utatenda kazi juu ya maskini wasikilizaji hawa, na ujalie Malaika wa Mungu wasogee tu karibu usiku wa leo.

196 Ni usiku wenye baridi. Wameteseka kwa muda mrefu, wameketi hapa kwenye baridi. Watunukie, Bwana, kwa kumponya kila mmoja. Tujalie, Bwana. Jalia huu uwe ndio usiku ambao kila mtu ataponywa.

197 Na sasa, Baba, mtume Malaika wa Bwana na asimame hapa karibu na mtumishi Wako mnyenyekevu na kunitia mafuta. Mimi. . .Wewe. . .Wewe unajua Bwana, siwajui watu hawa. Wao ni wageni kwangu. Lakini Wewe unawajua. Nami naomba ya kwamba utanisaidia, Bwana, na utanipa mambo hasa yaliyowaleta watu hawa hapa, wapate kujua ya kwamba umefufuka katika wafu, na unaishi hapa usiku wa leo, na uko tayari kuwasaidia; na mtazamo Wako kwao, leo, kama umefufuka katika wafu na kujithibitisha Mwenyewe katika nguvu, basi mtazamo Wako ni sawa na ulivyokuwa siku hiyo. Utujalie, Baba, na utubariki na utusamehe dhambi zetu. Katika Jina la Yesu tunaomba. Amina.

198 Sasa, kila mtu awe na kicho vile vile. Ninaamini hapa kuna leso labda ya kuombewa. Inaenda kwa mama fulani. Na hii hapa

nyingine, labda kitu kile kile. Nami nitaziombea hizi, na hiyo ni barua tu ya mtu binafsi kwangu.

Baba yetu wa Mbinguni, bariki leso hizi kwa madhumuni ziliyokusudiwa. Katika Jina la Yesu, ninaomba. Amina.

199 Sasa, sasa dada, wewe kaa sawa tu. . . Hiyo ni sawa, mnaweza tu kumwacha abaki papo hapo. Umbali hauna uhusiano wowote nao. Sababu pekee ya mimi kufika hapa, ni kwa sababu ni—ninajaribu kuwatenga na umati wote wa watu ili kuwasiliana nanyi.

200 Yesu hata aliwatuma wanafunzi Wake nje ilipomlazimu kuwasiliana na mwanamke huyo. Mnaona? Umewahi kusoma hiyo hadithi? Sijui kama uliwahi kuwazia kwamba kama ungeweza kusimama pale mwanamke huyo aliposimama. Je, hiyo si ingekuwa ya ajabu? Sikuzote uliwazia wewe—wewe. . . ingekuwa ajabu.

201 Laiti ungejua, dada yangu mpendwa, umesimama mahali pale pale. Um-hum. Hiyo ni kweli. Unajua, kama mwaminio sasa, kwamba jambo fulani linaendelea. Tangu nilipogeuka *huku* na kuanza kuzungumza, hisia halisi, tamu, nyenyekevu imekushukia. Je, hiyo ni kweli? Kama ndivyo, inua mkono wako juu kwa watu. Hiyo ni kweli. Maana kati yangu na wewe, labda hujawahi kuona picha yake, Nuru hiyo inatanda tu kati yangu na wewe.

202 Sasa hivi karibuni, Mungu akipenda, atakuwa. . . Labda uko katika awamu tatu tu. Hii ni awamu nyingine. Inanijia. Lakini ni Roho. Unaona? Iko katika ulimwengu mwingine.

203 Watu, hawajaondoka, wako—wako karibu nasi; Malaika na kadhalika. “Malaika wananinii. . . wa Mungu wanafanya kituo kuwazunguka hao wamchao.”

Mnamkumbuka Elisha kule Dothani asubuhi ile, wakati yule mvulana aliposema, “Loo, Wa-. . . majeshi ya Washami yametuzingira.”

Akasema, “Kuna wengi walio pamoja nasi kuliko walio pamoja nao.” Asingeweza kuona mtu yeyote. Akasema, “Mungu, yafumbue macho ya kijana huyu.”

204 Na wakati alipoyafumbua macho yake, karibu na yule nabii mzee kulikuwa—kulikuwa na Malaika wa moto na magari ya moto. Wao. . . Kulikuwa na ninii tu. . . Basi kuna wengi walio pamoja nasi kuliko walio pamoja nao.

205 Na huo ndio upeo sasa, kwa kuzaliwa. Labda hutawahi (Unaona?) kuona mambo kama hayo. Lakini unaamini hata hivyo. “Thawabu yao ni kubwa kiasi gani wale ambao hawajawahi kuona na bado wanaamini.” Lakini baadhi yetu tulizaliwa kwa ajili hiyo. Mungu huweka hilo kanisani, tangu kuzaliwa kwa mtoto mchanga. Manabii hawawekwi tu

na mwanadamu; ni karama ya kuzaliwa nayo; kote katika Maandiko, inayozaliwa tangu utotoni.

206 Na sasa, mwanamke ambaye amesimama mbele yangu… Nami…Kama kusanyiko bado linaweza kunisikia, Malaika wa Bwana anatulia. Nami ninajua ya kuwa ninasikika mahali fulani. Lakini anateseka na…anachofikiria ni ubavu uliovunjika. Uko ubavuni mwake. Ana uvimbe ubavuni mwake au fundo la aina fulani. Na ulisababishwa na mchanga kugonga ninii…kitu ambacho kilimgonga. Nacho kimesababisha hili kutokea. Je, hiyo ni kweli?

207 Sasa, sijui nililosema. Lakini si mimi niliyelisema. Hicho kilikuwa ni Kitu kingine kikilisema. Lakini lilikuwa ni kweli, lolote lililokuwa? Kama lilikuwa ni kweli, inua mkono wako.

208 Sasa, unajua ya kwamba Kitu fulani kiko hapa mbali na mwanadamu. Je, hiyo ni kweli? Kwa kuwa unajua kama hiyo ilikuwa kweli au la. Wewe ni shahidi wa hilo. Na kama ni kweli kwamba…Ameinua mkono wake kwa kusanyiko kwamba ni kweli. Na huyu mwanamke, akisimama hapa na Biblia imewekwa mbele yetu, mnajua asingesema jambo baya, na ni mwanamke Mkristo, pia, zaidi ya hayo. Hiyo ni kweli.

Basi kuna nini hapa? Yesu wa Nazareti, aliyefufuka katika wafu. Ni Roho Wake akitembea.

209 Sasa, njoo hapa, dada. Vyovyote ilivyokuwa, kama… Yesu alisema maneno haya, wakati Yeye…jambo la mwisho alilosema alipoondoka duniani: "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio." Marko 16. "Wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya."

210 Sasa, ingenibidi niwe mwaminio ili jambo fulani litukie kama tu lililotukia, kwa maana ni Mungu akikuthibitishia ya kwamba mimi ni mwaminio. Hiyo ni kweli? Nawe ni mwaminio, la sivyo kamwe nisingeweza kufanya hivyo. Imani yako ndiyo iliyofanya hivyo.

Sasa, sisi tukiwa karibu sana na Mungu, inakuwaje basi kama nikiweka mikono juu ya wagonjwa, inakuwaje? Utapona.

211 Sasa, Baba yetu wa Mbinguni, kwa kutii amri za Bwana wetu Yesu mpendwa, ninaweka mikono juu ya dada yangu na kuomba kwamba Maneno Yake yatimizwe. Na lolote linalomsumbua mwanamke huyu, jalia awe mzima, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

212 Mungu akubariki, dada. Nenda zako, ukifurahi na kushangilia. Sasa angalia, sahau tu hayo. Ikiwa ilikuwa ni ugonjwa, shida fulani uliyo nayo, au ikiwa ni jambo ambalo mtu mwingine anataka, chochote kilichokuwa, sahau tu, yote kukihusu. Yote yamekwisha; nenda tu, ukimsifu Mungu kwa ajili yake. Unaona? Itakuwa sawa. Amina.

Loo, Yeye ni wa ajabu. Najua mnafikiri nimerukwa na akili, lakini sivyo. Hapana, hapana, nina fahamu kabisa.

Vema, amini tu. Sawa, ni. . .? Hebu huyu mwanamke atoke hapa. Njoo moja kwa moja mbele, dada.

213 Sasa, nadhani mimi na wewe hatufahamiani, pia, mmoja kwa mwingine, sivyo? Mimi na wewe pamoja, tumeachana kwa miaka kadhaa, na sisi ni. . . Bali tu—tuna Bwana Yesu yeye yule, sivyo, dada? Sasa, sikujui, sijawahi kukuona. Lakini Yesu anajua yote kukuhusu.

214 Nawe umesoma katika Biblia, ambapo huko nyuma katika Agano la Kale, manabii walifanya hivyo. Naye Mungu akaahidi jambo lile lile. Na aliye mkuu kuliko manabii wote, na wafalme wote, na Bwana, na Mwalimu wao, alikuwa ni Yesu. Alipokuwa hapa duniani, Yeye alifanya tu hivi, kama, jambo lile lile; ila kubwa zaidi. Kisha akaondoka na kusema, "Mambo yale yale nifanyayo ninyi nanyi mtayafanya, hata ukamilifu wa dahari." Kwa hiyo ni Yesu tu katika Kanisa Lake, sivyo? Ikiwa ni. . .

215 Sasa sijui, wala nisingeweza kukuponya; kama wewe ni mgonjwa, sijui. Lakini ikiwa wewe ni mgonjwa, nisingeweza kukuponya. Ingembidi Yesu kukuponya, sivyo? Na. . . Lakini atakuponya kama utaamini. Sasa, Yeye ananinii tu. . . Kupitia kujua. . .

216 Sasa, vipi kama Yeye angalikuwa amesimama hapa na suti hii ambayo Yeye alimfanya Ndugu Gardner kunipa? Sasa, vipi kama. . .? Kama angalikuwa amesimama hapa amevaa suti hii, sasa asingeweza kusema, "Sasa, njoo hapa, nitakuponya." Hapana, asingefanya hivyo. Kama angefanya, ingembidi kulighairi Neno Lake. Angesema, "Mwanangu, hivi huamini nilifanya hivyo nilipokufa pale Kalvari, nilinunua uponyaji wako?"

Ungesema, "Naam, Bwana."

Kisha angesema, "Kwa kadiri ya imani yako basi, na iwe kwako." Hiyo ni kweli?

217 Au, vipi kama ingetokea kwamba Baba angemwonyesha, na kumwambia, angeweza. . . anaweza kukwambia shida yako au kitu kingine kama hicho, sivyo? Huenda angeweza kufanya hivyo, lakini hivyo ndivyo tu angeweza kufanya. Sasa, Yeye. . . Hilo ndilo jambo lile lile alilo usiku wa leo, akifanya kazi tu kupitia kwa wanadamu.

218 Sasa, amini kwa moyo wako wote na hakika Yeye atakuponya. Ninaamini Yeye atakuponya. Sivyo, mama? Je, huamini atakuponya? Bila shaka atakuponya.

219 Mungu anisaidie nifanye jambo la kuinua imani yako. Ninaona jambo moja, huyo mwanamke, kama kusanyiko lingali linanisikiliza, kuna kivuli karibu na huyu mwanamke. Yeye ni mahututi sana, sana. Ana tatizo katika figo lake. Hiyo ni kweli.

Na hiyo ni kansa kwenye figo. Na pia ana yabisi kavu, kwa sababu ninamwona, ni vigumu kwake kusogea nyakati fulani.

Hilo ono linaonekana kufifia. Mambo hayo ni kweli hata hivyo, sivyo? Ni ya kweli.

220 Unaamini sasa? Huyu mwanamke ndiye mwamuzi. Hilo ono lilionekana kidogo linafifia. Hebu kidogo, hebu nizungumze naye tena, kwa ajili tu ya kuwasiliana na nafsi yako, dada. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

221 Sasa, nitazame kwa muda kidogo tu. Ilionekana kana kwamba kuna kitu anachotaka. . .Ninakuona kwa njia fulani; unajaribu kusogea, ama, kuangalia, ama, hapana, inahusu mkono wako. Kwenye—kwenye mmoja wa mikono yako, chini ya mkono wako, una mahali. Ni mkono wa kushoto. Yesu anaweza kuponya huo, pia. Unaamini hilo? Ni kivimbe, ambacho ni uvimbe, na uko papo hapo chini ya mkono wako wa kushoto. Lakini Yesu Kristo anaweza kukuponya. Unaamini hilo? Basi njoo hapa. Amini sasa. Twaweza kuomba?

222 Baba yetu wa Mbinguni, ninaweka mikono juu ya mwanamke huyu, nami ninaomba ya kwamba kama vile kipofu Bartimayo alivyosimama pale na kufumbuliwa macho yake, jalia yeye pia, Bwana, apokee uponyaji wake, na vivuli hivi vya mauti viondolewe kwake. Jalia aende na awe mzima. Ninaomba baraka hii kwa ajili ya dada yangu, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

Mungu akubariki, dada. Nenda zako, kwa furaha na kushangilia, na kumshukuru Mungu, na uwe mzima.

223 Vema, hatufahamiani, nadhani, dada. Na. . .Lakini Mungu anatujua sote wawili, sivyo? Anatujua sote wawili.

224 Sasa, kama kulikuwa na chochote. . .Kama ningelikuwa na namna fulani ya uponyaji ama chochote kile. . .Jambo la kwanza, kama ningesema hivyo, ningekuwa nimekosea. Ningeyakiuka Maandiko. Lakini kama kweli nilikuwa nao, tuseme kama kweli nilikuwa nao, na kama nilikuwa daktari, na nilijua tatizo lako, halafu nisikuponye, ningekuwa mnafiki; naam, bwana; kama ningeweza kukusaidia, wala nisikusaidie. Lakini jambo pekee ninaloweza kufanya, ni vile tu Yeye angeniambia. Na hiyo ni kwa imani, imani yako katika Kri-. . .

225 Jambo fulani lilitukia basi; sasa, kila mtu awe na kicho kabisa. Mtu fulani alikuwa akiomba. Loo, hili hapa. Mungu asifiwe. Asante, dada, kwa kuomba. Niliyasikia maombi yako. Yesu aliyasikia pia. Malengelenge yako yatakuacha sasa, unayeketi papo hapo umeinua mkono wako namna *hii*, mama hapo, uliyeketi umeinua mkono wako. Sasa wewe. . .Naam, unaweza kwenda zako sasa ukishangilia; ameyasikia maombi yako. Asante, dada, kwa ajili ya imani yako katika Mungu. Amina. Yeye si ni wa ajabu, dada? Imani yako inafanya hivyo.

Sasa, iweni mkiomba. Nawe endelea kuomba, dada. Ninyi nyote, iweni tu katika maombi.

Sasa, huyu mama akiwa mgeni kwangu; sasa, nitazungumza nawe tu, kama mtumishi Wake . . .

226 Inaendelea kujongea katika kusanyiko. Kuna imani inayotokea huko nje. Unaona? Wakati mwingine sijui ni nini; inanibidi tu kufanya vile Yeye asemavyo. Roho wa Bwana anapoanza kusonga, inanibidi tu kusonga anavyosogea nami. Mnaona? Yote ni jambo moja, mimi . . .

227 Huyo hapo, juu ya mwanamke ambaye ana wasiwasi sana, anayeketi pale pale. Naye mumewe anaegemea kwake. Anaugua henia. Nao wote wawili wanaomba kuponywa. Hiyo ni kweli? Ninyi ni mume na mke. Ninawaona nyote wawili mkiwa kwenye chumba kimoja. Vema, wekeaneni mikono.

228 Baba wa Mbinguni, katika Jina la Yesu, jalia waponywe. Imani yao, Bwana, imekugusa Wewe na kusababisha hili. Katika Jina la Yesu, naomba wapate kuponywa. Amina.

Mungu awabariki, ndugu na dada yangu wapendwa. Imani yenu imefanya jambo hili, imani yenu pekee.

Ikiwa unaweza tu kuamini. Loo, jamani, Yeye si ni wa ajabu?

229 Kuna mwanamume mwingine na mke wameketi papo hapo nyuma, naye mwanamke huyo anaugua henia, anayeketi moja kwa moja mstarini pamoja nao. Naye mwanamume huyo ni . . . ana shida ya kusikia na pia ana bawasiri. Nao wameketi pale pale juu, huyo mwanamke na mwanamume. Mmeponywa, nyote wawili. Yesu Kristo anawafanya . . .

230 Unanisikia sasa, sivyo ndugu? Masikio yako yamefunguka. Mungu asifiwe. Hiyo hapo, Bwana wetu Yesu katika rehema Zake nyingi; ameketi pale akiwa na imani; ni kitu gani kinachofanya hivyo? Imani ile ile iliyokuwa kwa kipofu Bartimayo. Ninyi nyote mnapaswa kuamini.

231 Inaning'inia juu ya huyo mama, uh-huh, kwenye machela. Uh-huh. Ninashangaa juu ya imani yake. Yeye ni mgonjwa sana: ugonjwa wa pumu; ana TB; yabisi kavu. Hiyo ni kweli, sivyo, ewe msichana, wewe uliye ndani ya . . .? Hiyo ni kweli. Mama, kama ungeweza tu kuamini, na kuniamini mimi kuwa ni nabii wa Mungu: Mara tu ibada hii itakapokwisha, chukua hicho kitanda kidogo ukikunje uende nyumbani. Hmm. Uwe na imani. Amini.

Sasa, mama, hebu kidogo. Samahani. Yanipasa tu kuhama jinsi Hiyo inavyohama.

232 Msisogee-sogee, mtu yeyote. Mnaona? Ninyi . . . Malaika wa Bwana ni Nuru. Ni Nguzo ya Moto (Mnaona?), Nuru tu, Nuru kama zumaridi inayowaka, Nayo huhama. Na—nanyi mkisogea, wakati mwingine, ni sisi, nafsi ya kibinadamu. Ninyi nyote ni kama mko chini ya udhibiti, basi mkisogea . . . Nami najua pale ambapo mwenye kushuku ameketi; ninajua mahali waaminio

wameketi. Sina budi kuangalia hasa. Wakati hiyo inapohama, hayo ni mapambano, ni katika maisha ya kiroho. Uh-huh.

233 Sasa, hapa, i—inaonekana kana kwamba mngeweza kuona hilo. Naona damu ikidondoka. Inatoka kwa mtu huyo anayeketi pale pale, kama safu tatu nyuma, anayeketi pale, ana damu inadondoka kutoka kwenye mapafu. Ana shida, mdondoko wa damu. Naam, bwana.

234 Sasa, amini. Usitie shaka, bali uamini, naye Yesu Kristo atakuponya. "Kama unaweza kuamini, mambo yote yanawezekana." Sasa, unaamini, dada?

235 Mwanamume anayeketi upande huu kule anaugua ugonjwa wa tezi kibofu, anayeketi papa hapa nyuma, kwa namna fulani akinitazama, kidogo ni mzee. Kama unaweza kuamini, ndugu yangu mpendwa, utakuacha wala hautarudi tena. Ninamwamini Mungu kwamba una imani yako na unaamini kwa moyo wako wote. Utapokea ulichoomba. Ajabu!

236 Sasa, huyo mama, samahani, dada, sina budi kuninii... Ninaona milima mikubwa mirefu ikija mbele yangu, milima mikubwa mno. Imefunikwa na theluji kote.

237 Loo, uko hapa kwa niaba ya mtu mwingine, na mtu huyo anaishi tu kwenye mlima. Ni Denver, Colorado. Na huyo ni mwanamume, na ni wa jamii yako. Na ni m—mtu ambaye hajaokoka; yeye si Mkristo; mtu huyo amezungukwa na giza. Naye amekuwa...amekuwa katika namna fulani ya hospitali na akafanyiwa upasuaji wa ubongo. Nao wameijeruhi mishipa, naye...ni mshipa wa usawa; hawezi kutembea. Mnajaribu ku-...hawezi kuketi au kuendelea *hivyo*. Na ni shemeji yako. Hivyo ndivyo hasa.

238 Sasa, hiyo leso, uliyofutia machozi machoni pako, mtumie katika Jina la Bwana Yesu, na hebu na aponywe kwa...

Amini tu. Usiwe na shaka. Amini, nawe utapokea. "Ikiwa unaweza kuamini, utapokea." Biblia ilisema kwamba ungepokea.

239 Ninaendelea kumwona mwanamke Mhispaniola amesimama angani, moja kwa moja kupitia hapa, mahali fulani. Siwezi kujua mahali ilipo, kwa hiyo endelea tu kuomba, popote mlipo. Hata inawezekana uko nyuma yangu. Sijui. Lakini tafadhalini iweni na kicho na heshima na mtulie kwa muda mfupi tu.

Loo, tunaye Bwana Yesu wa ajabu jinsi gani. Jinsi alivyo mwema, jinsi alivyo wa thamani. Anafanya mambo yote vizuri.

240 Sasa, kama naweza kupata usikivu wa maskini mama huyu, hapa, ambaye amesimama mbele yangu. Dada, usilie. Unaona? Bartimayo labda alilia. Lakini ikiwa unahitaji kitu chochote, Yesu yuko hapa kukupa kila kitu unachohitaji.

241 Sasa, mimi ni ndugu yako, na ningekwambia tu ukweli, dada. Nawe unajua kuwa sikujui, wala kujua chochote

kukuhusu. Una—unajua hilo. Sivyo, dada? Lakini, je, huwezi kuamini kwamba ninasema ukweli kuhusu Biblia? ya kwamba Yesu ni yeye yule jana, leo na hata milele.

242 Vipi kama ulikuwa umesimama katika Uwepo Wake? Angejua kukuhusu, kile ambacho Baba angemfunulia. Hiyo ni kweli? Yule mwanamke aligusa vazi Lake, ila Yeye asingeweza kulisimulia mpaka Baba alipomwonyesha. Alisema, "Kama vile tu Baba anavyonionyesha Mimi, ndivyo nifanyavyo."

243 Jamani, ni imani ya ajabu jinsi gani inayojongea kwenye kusanyiko hili. Loo, kama wewe. . . Nikiondoka hapa, majuma kadhaa, ninyi watu mtagundua kuwa mmepata afya. Mnaponywa. Siwezi tu kuwataja. Ni kila mahali tu, inavyoonekana. Inaonekana kama tu. . . Ninatazama pande zote, na kila kitu kinageuka kuwa nuru, kwa njia hiyo. Na halafu, imani kubwa sana, mnaponywa. M—mtautambua. Ninii, labda. . . Ninyi angalieni muone, wachungaji, kama watu wenu hawaji, wawaambie ni wao—wao waliponywa hapa, na hata hawakuwa karibu, hakuna mtu aliyezungumza nao wala chochote kile. Wanaponywa kwa vyovyote vile. Huwezi kuwatambulisha wakati wakiwa wengi sana sasa.

244 Kwa hivyo labda pamoja na dada yetu hapa, una. . . Ninaona shida fulani kooni mwako. Una ugonjwa wa koo. Hiyo ni kweli. Nawe una wasiwasi sana, umefadhaika. Na ndio kwanza jambo fulani likupate, kama mshtuko wa moyo. Ulipata mshtuko wa moyo hivi majuzi tu, na ukakuacha mnyonge sana na mwenye wasiwasi. Njoo hapa.

245 Mpendwa Baba wa Mbinguni, Mwanzilishi wa Uzima na Mpaji wa kila thawabu njema, tuma baraka Zako juu ya huyu, Mjakazi wako mnyenyekevu, Bwana, na umponye, na umfanye mzima kabisa. Ninaomba, katika Jina la Yesu, Mwana wa Mungu. Amina.

246 Sasa nenda. Usitie shaka hata kidogo, dada. Umebarikiwa na Mungu sasa. Nami nimeomba, na ninaamini kwamba ninapata kile ninachoomba. Je, huamini hivyo? Basi nenda, ukakidai, na utapata ulichoomba. Amina.

247 Mwamini Mungu. Unaamini? Sasa tafadhalini. . . Na—nadhani labda mimi. . . Hivi mimi. . . Naam, ninachelewa, labda. Vema, hebu kidogo, kila mtu awe ninii kabisa. . . Ninajaribu kuwafanyia kazi, kwa ajili ya Mungu, kwenu, kama mtatulia tu na msisogee kwa dakika moja. . .

Hebu niongee na mwanamke huyu, hapa. Huyu ndiye mgonjwa, bwana? Bwana akubariki, mama. Unaongea Kiingereza? Hilo ni zuri sana.

248 Sasa, mnaona, jambo hili halina budi kuwa la kicho sana. Mnasema, "Ndugu Branham, hilo lina uhusiano gani nalo?" Mwingi sana. Yesu, wakati mmoja, akimponya mtu, alimtoa nje

ya makutano ya watu, akampeleka nje ya mji, akamwombea. Hiyo ni kweli?

249 Na wakati mmoja wakati binti Yairo alipokuwa amekufa, watu wote walikuwa wakilia na kupiga makelele, Naye akawatoa, kila mmoja, nje ya nyumba. Hiyo ni kweli? Mnaona? Naam, hii. . . Wewe ni—wewe ni—wewe ni—wewe ni. . . jinsi unavyosogea, kitendo chako, unaona, uko katika ulimwengu mwingine.

250 Oh, ninakupenda kwa moyo wangu wote. Laiti ungempokea tu Bwana wangu Yesu sasa hivi. Ungeona moja ya mambo makubwa zaidi uliyowahi kuona maishani mwako. Lakini amini tu.

251 Sasa, huyu hapa mwanamke, labda ni Mhispaniola. Si—sijui mimi. Lakini Mungu anamjua. Simjui mimi. Ikiwa Mungu, Baba yetu wa Mbinguni, atazungumza na mwanamke huyu kupitia kwa Roho Mtakatifu, atumie tu midomo yangu, ninapojisalimisha Kwake, na kunijulisha kilichomleta hapa mwanamke huyu Mhispaniola, ninyi nyote, kwa wakati mmoja, mtasema, "Hilo litanitosha mimi, milele. Sasa hivi, basi, nitamwamini Bwana Yesu Kristo na kumkubali"? Mtafanya hivyo? Vema, basi tungeweza kuomba, na kila mtu angeponywa.

Tayari umeponywa. Ninamaanisha, ukubali. Unaona? Unapoukubali, hapo ndipo tunapojua.

252 Vema, dada, Bwana Yesu na akujalie. Wewe, Mhispaniola, na mimi, Mwairishi, na kuachana kwa miaka kadhaa na—na kadhalika, hatufahamiani. Lakini Yesu anatujua, sivyo? Anajua yote kulihusu.

253 Una u—ugonjwa wa fadhaa, ugonjwa wa tumbo, hiyo ni kweli, maumvivu ya jicho lako, pia. Hiyo ni kweli. Hutoki hapa. Wewe hutoki eneo hili. Hapana, unatoka sehemu nyingine inayoitwa El Monte, California, kitu kama hicho. Hiyo ni kweli. Na jina lako ni Naomi. Hiyo ni kweli. Moore ndilo jina lako la mwisho. Na nambari ya nyumba yako ni 502, kitu kama hicho, Mtaa wa Mullhall. Hiyo ni kweli. Hiyo ni kweli? Sasa, rudi vizuri. Yesu anakuponya.

Ee Mungu, uturehemu, ninaomba, kupitia Jina la Yesu.

Mnaamini?

254 Bwana, unataka kwenda kula chakula chako cha jioni? Vema, nenda ukajipatie hambaga nzuri na kubwa ule. Ugonjwa wako wa tumbo ulikuacha. Amina. Nenda, ukawe. . .

Njoo. Kamwe hutafanyiwa upasuaji; uvimbe tayari umetoweka. Nenda zako mbio, ukishangilia.

255 Tuseme, "Bwana asifiwe." Roho Mtakatifu yuko hapa kama ungeweza tu kuamini. Jambo ndilo hili. Hii ndiyo inahitajika kulifanya.

256 Ikiwa utaamini, moyo hautakusumbua tena. Endelea tu kutembea, na kushangilia, na kumshukuru Mungu kwa moyo wako wote na nafsi. Hebu tuseme, "Bwana asifiwe."

257 Ikiwa unaweza kuwa na imani . . . Hisia za kigeni, niliposema kuhusu ugonjwa wa tumbo kwa mtu huyo, sivyo? Sasa, nenda ukafanye vivyo hivyo. Kula chakula chako cha jioni, katika Jina la Yesu.

258 Je, mnaamini huko nje? Je, mnataka kuponywa, kila mmoja wenu, sasa hivi? Vema, basi fanya hivi: Inamisha kichwa chako, kwa muda kidogo, sasa, wewe rudia maombi haya. Ombeni maombi ninayosema:

259 Mpendwa Baba wa Mbinguni, sasa ninaamini kwamba Yesu, Mwanao, amefufuka katika wafu, na amenisamehe dhambi zangu, na kuponya ugonjwa wangu. Ninakubali sasa hivi. Ninaamini ya kwamba Wewe uko hapa katika umbo la Roho, ukifanya mambo yale yale uliyofanya, ulipokuwa hapa katika mwili. Nami nakukubali Wewe kama Mponyaji wangu. Nisaidie, Bwana, nisiwe na shaka tena.

260 Sasa, wewe nyamaza tu kabisa, jifungie ndani pamoja na Mungu. Inamisha tu kichwa chako chini. Hayo ndiyo maombi yako.

261 Sasa, kwa imani tu, mwangalie Yeye. Kwa macho ya imani sasa, huku macho yako ya kimwili yamefumbwa, mtazame Yeye; hebu wazia, Huyo hapo amesimama, papo hapo kando yako; mikono Yake imenyooshwa. Sasa, kuna jambo moja tu la kukuzuia kuipokea. Moja kwa moja juu yako kivuli cheusi kimening'inia. Huyo ni Shetani, mwenye kushuku, akijaribu kusema, "Vema, ningeninii . . . kitu kingine."

262 Sasa, nitakemea shaka hilo, kitu hicho kinachofanya . . . kingekufanya utilie shaka. Hayo ni maombi yangu. Sasa, wewe jifungie tu ndani pamoja na Mungu ninapokuombea, nikiamini kwamba nguvu za Mungu za uponyaji zinakuja moja kwa moja ndani yako kwa imani yako mwenyewe sasa hivi. Nguvu za Mungu za uponyaji zinaingia moja kwa moja ndani yako kwa imani kwamba unaipokea.

Kansa zote zinatoka. Ugonjwa wa tumbo unaondoka. Ugonjwa wa kike unaondoka. Magonjwa yote yanaondoka.

Sasa, Baba wa Mbinguni, wamekiri. Wameleta shida yao Kwako. Na sasa ninawaleta Kwako.

Na sasa, pepo huyu wa mashaka ambaye angening'inia juu ya watu, ambaye angewafanya watilie shaka:

263 Shetani, umeshindwa vita. Kwa miaka mingi umewafunga wanadamu katika mashaka, lakini Mungu, kwa rehema Zake, alitutumia Nuru. Nawe ni mdanganyifu. Tena umefichuliwa, wala huna haki za kisheria. Yesu Kristo Mwana wa Mungu alikuvua pale Kalvari kila kitu ulichopata kuwa nacho. Nawe

ni mdanganyifu tu. Nasi tunakupa changamoto, kupitia kwa Damu ya Yesu. Wala huwezi kutufanya tuwe na shaka tena, kwa hiyo toka kwa watu hawa, na uwaondokee, na uhame kwenye maskani hii, usiku wa leo. Ninakuapisha, kwa Jina la . . . Yesu Kristo, Mwana wa Mungu aliye hai, kwamba kila shaka limwondokee kila mtu, naye Yesu Kristo anawafanya kuwa wakamilifu kabisa. Kwa ajili ya utukufu wa Mungu, ninaomba haya, katika Jina la Yesu. Pia, Shetani, unakemewa. Toka ndani yao.

55-1115 Bartimayo Kipofu
Tent Meeting
San Fernando, California Marekani

SWAHILI

©2022 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org